# Nipashe

Jumamosi Oktoba 5, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580041

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Mwili wa mwanafunzi wenye deni mil. 26/- hospitalini waruhusiwa

UKURASA 3




UKURASA 13


## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MWILI WA MWONGOZAJI WA WATALII WAOPOLEWA**

ALIYEKUWA nahodha wa mtumbwi wa Kampuni ya kitalii ya Wayo Africa, Samweli Mhina (33), amepatikana akiwa amekufa na mwili wake ukiwa chini ya maji...

UKURASA WA 3

**WATUHUMIWA 50 WAJITOKEZA KULIPA WASAMEHEWE MAKOSA**

WATUHUMIWA 50 wa makosa ya uhujumu uchumi wamejitokeza kuomba kukiri makosa yao kwa ajili ya kulipa na kusamehewa...

UKURASA WA 4

**WAZIRI APIGA 'STOP' UJENZI WA VIWANDA MAKAZI YA WATU**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amepiga marufuku utoaji vibali vya ujenzi wa viwanda kwenye maeneo ya makazi ya...


## Lugola atumbua vigogo polisi

UKURASA 3

# JPM abariki bakora za RC

**NI** kwa kuwacharaza wanafunzi watukutu, aagiza waliohusika wafukuzwe shule...*Endelea ukurasa wa 2*



Wakazi wa jiji, wakijipatia riziki kwa kuwaosha miguu watu waliotoka katika soko la Mabibo maarufu kama Mahakama ya Ndizi, jijini Dar es Salaam jana, lililojaa matope mengi yaliyosababishwa na mvua zilizonyesha jijini humo. Gharama ya kuosha inaanzia 200/- hadi 500/- kwa mtu mmoja. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Mkuu wa Mkoa ahamasisha maandamano ujenzi mitaro

UKURASA 2


**MICHEZO** "MUUAJI" YANGA AITWA KUONGEZA NGUVU STARS UK. 31

**MAONI, KATUNI UK.6**

# JPM apongeza bakora za RC

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amempongeza Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kwa uamuzi wa kuwatandika viboko wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kiwanja iliyoko Chunja mkoani Mbeya na kuagiza wote wafukuzwe shule.

Akizungumza jana mkoani Songwe katika ziara ya kikazi, alisema juzi alimpigia simu Chalamila kumpongeza kwa kuwachapa wanafunzi 14 viboko vitatu kila mmoja.

"Leo (jana) nilikuwa naongeza na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, nikamwambia ninakupongeza kweli kwa kuwatandika wale viboko, nikamwambia uliwatandika viboko vichache," alisema.

"Haiwezekani serikali tunatoa mabilioni ya (fedha) kujenga madarasa na shule halafu mtoto anakwenda kuichoma, nikamwambia hao watoto fukuza wote. Kwa hiyo kidato cha tano na sita wa shule ile wote wamefukuzwa na bodi imevunjwa kwa sababu huo ni uzembe wa bodi ya shule." "Eti haki za binadamu, haki za binadamu watoto wawe na viburi vya kipumbavu! Ni lazima tufike mahali tuache mambo ya mchezo tufanye maendeleo. Hizi fedha zimechangiwa na wazazi maskini watoto wetu wakasome. Unakwenda pale unanyang'anywa simu unachoma jengo, nidhamu ya namna gani hii?" alihoji na kuongeza:

"Hao haki za binadamu wakayajenge mabweni. Nimesema ili wanafunzi hao warudi shuleni lazima baba zao walipe ili mabweni yale yajengwe na wale wengine ambao walihusika kabisa wapelekwe jela."

Rais Magufuli aliueleza mkutano huo kuwa anayaeleza hayo si kwamba hana huruma.

"Nina upendo mkubwa tena nimekuwa mwalimu nina fahamu ninawaomba wazazi na viongozi muache mambo ya kusema akipigwa viboko. Nafikiri kama kuna mahali tulikosea ile sheria, ikafanyiwe marekebisho wawe wanatandikwa viboko.

"Ati mkuu wa mkoa ametandika viboko maana yake nini? Hata Ulaya wanatandikwa, nimekaa Ulaya kuna shule ambazo wanazisomea wao wakubwa wanatandikwa viboko lakini kwenye shule ambazo wanataka wavuta bangi hawatandiki viboko," alisema.

Rais Magufuli alisema kiboko kinafundisha ndiyo maana watoto wa sasa wanarudi nyumbani hawasomi.

Rais Magufuli alisisitiza kuwa haiwezekani kwenda bila viboko na kumgeukia David Silinde (Mbunge wa Momba) na kumuuliza kama alikuwa hatandikwi viboko enzi zake. "Ulipigwa viboko ndiyo maana ulifika ukawa mbunge, ndiyo maana umeingia bungeni wala huitukani CCM kwa sababu unajua unatekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ninakupongeza sana," alisema.

Alisema Silinde aliwakilisha kwenye Bunge la Afrika baada ya kupigiwa kura na wabunge wa CCM.

**AWAPONGEZA WAPINZANI**

Rais Magufuli alisema anawapongeza wabunge wa vyama vya upinzani wanaoshirikiana na wabunge wa CCM katika kuleta maendeleo.

"Maendeleo hayana chama, chama kitakacholeta maendeleo mazuri ni chama ambacho mwenyekiti wake ni wa CCM (ambaye ni Rais Magufuli)," alisema.

**UAMUZI WA RC**

Awali, Chalamila alitangaza kurejesha nyumbani wanafunzi

INAENDELEA UK. 8



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (katikati), akisisitiza jambo jana alipokuwa anazungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kiwanja wilayani Chunya kuhusu uamuzi wake wa kuwatimua wanafunzi wa Kidato cha tano na sita kufuatia kuchoma moto mabweni ya Shule hiyo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mkuu wa Mkoa ahamasisha maandamano ujenzi mitaro

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amesema atahamasisha wananchi wa kata tano za wilaya ya Ilala, kufanya maandamano kwenda Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kudai ujenzi wa mifereji eneo la Buguruni Mivinjeni.

Alitoa kauli hiyo jana katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo wilayani Ilala baada ya kuzungumza kwa simu na Mratibu wa Miradi ya Uboreshaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP) wa Tamisemi, Emmanuel Ndyamukama, baada ya kupewa majibu yasiyoridhisha.

Makonda alisema atafanya maandamano hayo Oktoba 10, mwaka huu, kama bado Tamisemi itakuwa haijaanza ujenzi wa mitaro hiyo.

"Majibu ya Ndyamukama ni kwamba mradi huo haujakwama bali kilichofanyika sasa ni makubaliano kati ya Wizara ya Fedha na Mipango na Tamisemi yanayoendelea," alisema Makonda.

Makonda alisikika akizungumza kwa njia ya simu akisema: "Tuna miezi sita bado wanajiridhisha nini? mvua zinakuja, hapa tuna mifereji na wewe ni shahidi nimepigia kelele muda mrefu. Wananchi hawamjui anayehusika zaidi ya Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na jumba bovu linamwangukia Mkuu wa Mkoa (Makonda)."

"Naomba jambo moja, leo (jana) ni Oktoba 4 na ikifika Oktoba 10 kama mkandarasi hajaanza na mifereji hii ipo, mimi nahamasisha maandamano ya kata zote tano tunakuja huko ofisini kwenu. Umenielewa? mwambie bosi wako, Katibu Mkuu Tamisemi na Waziri wa Tamisemi kwamba ikifika tarehe 10 Makonda anakuja na wananchi wa kata zote tano," aliongeza

Makonda alisema haiwezekani watie saini mkataba na kuingia makubaliano na kuahidi wananchi halafu bado kazi haifanyiki huku wanaobeba mzigo ni wao na wote wakifika wanaona Makonda ameshindwa kazi wakati si kweli.

# Mwili wa mwongoza watalii waopolewa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

ALIYEKUWA nahodha wa mtumbwi wa Kampuni ya kitalii ya Wayo Africa, Samweli Mhina (33), amepatikana akiwa amekufa na mwili wake ukiwa chini ya maji.

Nahodha huyo alibeba mtalii Dk. Rosenbever Heike raia wa Ujerumani, kwa ajili ya kumtembeza ndani ya Ziwa Momela kwenye Hifadhi ya Taifa ya Arusha.

Mtumbwi huo ulizama Oktoba Mosi, mwaka huu, baada ya kutokea kimbunga kikali mkoani hapa.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, alisema jana kuwa mwili huo ulipatikana baada ya kupata wazamiaji wa kikosi cha Zimamoto kutoka Dar es Salaam, waliowasili juzi usiku na kufanya kazi hiyo kwa saa moja na nusu.

"Oktoba 4 (jana) majira ya saa 3:00 asubuhi walikwenda ziwani kuanza kazi ya uokoaji na baada ya saa moja na nusu walifanikiwa kutoka na mwili chini ya maji ya ziwa hilo," alisema.

Alisema jambo hilo ni la kumshukuru Mungu kwa kuwa lilikuwa hitaji la ndugu wa marehemu kuwa mwili wa ndugu yao upatikane na serikali imefanikisha hilo.

Muro alitoa pole kwa wafiwa na kutoa wito kwa wananchi kuchukua tahadhali pindi wanapopata taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa.

"Tusisubiri matukio yatokee, tuchukue tahadhali katika jambo lolote, kwani hatujuwi shida itatokea wakati gani. Pamoja na hayo mwili huu umekaa ndani ya maji siku nne sasa na leo tumehitimisha baada ya wazamiaji kuupata chini ya maji," alisema.

Baba mdogo wa marehemu, Denisi Mhina, alishukuru jitihada za wazamiaji walioibua mwili wa ndugu yao chini ya maji na wamepeleka kuhifadhi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mount Meru kwa ajili ya taratibu za mazishi.

Msaidizi wa uokoaji Wilaya ya Arumeru, Sajenti Otorosi, alisema wameupata mwili kupitia msaada wa wazamiaji kutoka Dar es Salaam.

Hata hivyo, alisema kazi hiyo haikuwa rahisi kwa sababu walihitaji uzamaji ndani ya maji lakini kutokana na vifaa vya kisasa walivyokuwa navyo wazamiaji, waliupata mwili kwa haraka.

Oktoba Mosi majira ya saa 8:45 mchana kwenye kijiji cha Olkungw'ado wilayani Arumeru, Mtumbwi uliokuwa na mtalii Heike na nahodha Mhina, ulipigwa na dhoruba baada ya kimbunga kikali kutokea ghafla wakiwa ziwani humo na kuzama, huku mtalii huyo akiokolewa.

## HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akiangalia korosho zilizotoka kwenye mradi wa shamba la korosho la Masigati wilayani Manyoni, mkoani Singida, wakati alipokagua mradi huo, jana. Kutoka kushoto ni Mke wa Waziri Mkuu, Mary Majaliwa, Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Rehema Nchimbi na Meneja wa Kanda ya Kati, Bodi ya Korosho, Ray Mtangi. **PICHA: OWM**

# Mwili wa mwanafunzi wenye deni mil. 26/- hospitalini waruhusiwa

**Na Beatrice Moses**

MWILI wa Mwanafunzi Mwanaidi Nakari (16) wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari ya Makurumla, jijini Dar es Salaam, uliokuwa umezuiwa kwa siku tano katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili - Mloganzila kutokana na deni la Sh. milioni 26.8, umekabidhiwa kwa familia yake.

Mwili huo umekabidhiwa kwa familia ambayo ilijichangisha na kupata kiasi cha Sh. milioni tano baada ya kupewa msamaha wa zaidi ya Sh. milioni 21.8.

Shangazi wa marehemu, Asha Mkembe,

INAENDELEA UK. 8

# Watuhumiwa 50 wajitokeza kulipa wasamehewe makosa

**Na Waandishi Wetu**

WATUHUMIWA 50 wa makosa ya uhujumu uchumi wamejitokeza kuomba kukiri makosa yao kwa ajili ya kulipa na kusamehewa.

Huku watuhumiwa hao wakijitokea, wengine watatu wametiwa hatiani mkoani Arusha kwa kutorosha madini na kuhukumiwa kulipa Sh. milioni 100.

Watuhumiwa hao wamekiri makosa ya utakatishaji fedha, kukutwa na nyara za serikali na kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Kati ya watuhumiwa hao 10 wanatoka katika gereza la Keko na 40 wako Segerea.

Naye Makamu wa Rais wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Michael Wambura, ameieleza mahakama kuwa amekubaliana na Mkurugenzi wa Mashtaka DPP, kuwa hana uwezo wa kulipa Sh. milioni 100 badala yake uwezo wa kulipa Sh. milioni 85.

Kutoka Arusha, watuhumiwa watatu wametiwa hatiani kwa kutorosha madini na kuhukumiwa kulipa faini na fidia ya Sh. milioni 200 au kwenda jela miaka mitatu kila mmoja.

Akitoa hukumu hiyo juzi iliyoanza saa 1:11 na kuisha 4:40 usiku katika Mahakama ya Wilaya ya

INAENDELEA UK. 8

# Lugola atumbua vigogo polisi wilaya

**Na Mwandishi Wetu,** NKASI

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amewaondoa katika nyadhifa zao viongozi wakuu wa Jeshi la Polisi wa Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa kwa madai ya kushindwa kumudu majukumu yao.

Lugola amechukua hatua hiyo baada ya kubaini kuwapo kwa wizi wa mara kwa mara wa mifugo wilayani hapa na pia ni siku tatu baada ya kuamuru askari wote sita wa kituo cha Majimoto wilayani Mlele kuhamishwa kutokana na kukabiliwa na tuhuma mbalimbali.

Pia ameagiza askari sita wa Kituo cha Polisi Namanyere na Kirando wilayani humo waondolewe kutokana na wananchi wengi kuwalalamikia kushindwa kuwasaidia wanaporipoti matukio mbalimbali. Badala ya kuwasaidia wamekuwa wakiwapuuza na kuwakatisha tamaa.

Akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara, mjini Namanyere juzi, Lugola alisema Mkuu wa Polisi wa Wilaya hiyo (OCD), David Mtasya, Mkuu wa Upelelezi wa Wilaya (OC CID), Emanuely Kajala na Mkuu wa Kituo cha Polisi Namanyere (OCS), Ramadhani Msangi, lazima waondoke katika wilaya hiyo kwa kuwa wameshindwa kuimudu kazi yao ipasavyo.

"Wananchi wa Namanyere, nimesikia malalamiko ya kutopata msaada kutoka Jeshi la Polisi pindi wanapotoa mara kwa mara taarifa ya kuibiwa ng'ombe 278 wa wamiliki tofauti katika kituo cha polisi. Wamekuwa hawasikilizwi, wanazungushwa, wanapuuzwa mpaka kiasi kikubwa cha ng'ombe kimepotea. "Wananchi 15 walioripoti polisi mpaka sasa hawajapata msaada. Hii haiwezekani na siwezi kukaa kimya. Viongozi hawa wameshindwa kazi na lazima waondoke waje wengine," alisema Lugola.

Aliongeza kuwa licha ya polisi hao kupokea malalamiko mengi vituoni, wanawaachia watuhumiwa wa wizi wa ng'ombe wa wananchi na kuonekana mitaani kiasi kwamba wananchi hao wanapatwa na hasira na kuanza kuichukia serikali.

Akitoa kero yake kwa Waziri, mkazi wa Namanyere, Felista Mkomo, alisema mwaka jana aliibiwa ng'ombe wake lakini walifanikiwa kuwakamata wawili ila wengine mpaka sasa hawajawapata na kwamba aliripoti tukio hilo kituo cha polisi lakini mpaka sasa hakuna chochote kilichofanyika na hakuna mwizi aliyekamatwa.

Aliongeza kuwa polisi hao wameshindwa kuwasaka mitaani watuhumiwa hao wa wizi, kiasi kwamba wizi unaendelea wilayani hapa na kuwafanya kukosa mahali pa kukimbilia kutoa malalamiko yao.

Akijibu kero hizo, Lugola alisema serikali haiwezi kuchezewa na mtu yeyote na kamwe haiwezi kuona wananchi wake wanateseka kiasi hicho.

Viongozi wa polisi wilaya wameshindwa kumudu kazi zao, wameshindwa kuwahudumia wananchi, hivyo wanapaswa kuondoka wilayani hapa na wataletwa wapya," alisisitiza Lugola.




## DC Kilolo awashukia wadaiwa Saccos

**Na Friday Simbaya,** KILOLO

MKUU wa Wilaya ya Kilolo, Asia Abdallah, ameagiza wadaiwa sugu katika Chama cha Kuweka na Kukopa (Saccos) cha Mazombe, kurejesha mikopo yao kabla ya sheria kuchukua mkondo wake.

Abdallah alitoa agizo hilo jana wakati wa kikao chake na wadaiwa sugu kilichofanyika katika mji mdogo wa Ilula, Kilolo mkoani Iringa.

Alisema ni vizuri watu wazingatie mikataba wanayoingia na Saccos wakati wa kukopa fedha kwa kujenga nidhamu ya matumizi ili kuzitumia katika malengo husika na kukuza uchumi wa mlengwa hatimaye kuzirudisha kwa wakati ili kutoa fursa kwa wengine kunufaika na mikopo hiyo.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa wilaya, dhamira ya serikali ni kuendelea kuweka misingi imara ya ushirika na kuona wanachama wake wananufaika na ushirika, hivyo si vyema kuona wanachama wachache wanajinufaisha kwa kukopa na kushindwa kurejesha mikopo yao.

Mkuu huyo wa wilaya aliongeza kuwa Mazombe ni miongoni mwa Saccos nchini zinazofanya vizuri lakini madeni sugu yanahatarisha chama hicho.

Alitoa muda kwa wadaiwa hao mpaka Desemba 30, mwaka huu, wawe wamerejesha madeni ili kunusuru chama hicho kufa huku akionya kuwa watakaoshindwa kufanya hivyo watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Naye Mwenyekiti wa Bodi wa Mazombe Saccos, Yohana Mwemutsi, aliwaomba wadaiwa sugu walipe madeni yao ya muda mrefu kwa zaidi ya miaka mitatu na kuongeza kuwa saccos ni mkombozi wao na wakulima.

Meneja wa Mazombe Saccos, Longino Ngwada, alimshukuru mkuu wa wilaya ya Kilolo, kwa kuhamasisha wadaiwa sugu kurejesha mikopo na kuongeza kuwa mpaka sasa wamefanikiwa kurejesha zaidi ya Sh. milioni mia moja.

Alisema mkuu huyo amekuwa msaada mkubwa kwao kwa kuhamasisha wadaiwa sugu na hatua hiyo imesaidia kupunguza madeni kutoa kwa wadaiwa.

Ngwada alisema madeni ambayo yako nje ni zaidi ya Sh. milioni mia nne na kwamba saccos hiyo ina wanachana 1,758 na wadaiwa sugu ni zaidi ya 200.

Pamoja na madeni hayo, Ngwada alisema mambo mengi mazuri yanafanywa na Mazombe Saccos kwa kuongoza mkoa mzima kwa kuwa saccos ya kwanza kufanya vizuri.



Aliyekuwa Mhasibu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Godfrey Gugai (kulia), akiwa chini ya ulinzi wa Askari Magereza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili kuahirishwa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waziri apiga ‘stop’ ujenzi wa viwanda makazi ya watu

**Na Munir Shemweta,**

MKURANGA

NAIBU Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amepiga marufuku utoaji vibali vya ujenzi wa viwanda kwenye maeneo ya makazi ya watu katika wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani.

Dk. Mabula alisema hayo juzi alipokutana na uongozi na watumishi wa sekta ya ardhi wakati wa ziara yake ya siku moja wilayani hapa kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya ardhi na kutatua migogoro ya sekta hiyo.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga lazima iandae Mpango Kabambe aioueleza kuwa utakuwa dira katika kuonyesha matumizi ya ardhi kwa kuwa maeneo kama viwanda, makazi na matumizi mengine yatakuwa yameonyeshwa na kuondoa ujenzi wa makazi holela.

Kuhusu urasimishaji, Naibu Waziri aliitaka Mkuranga kuharakisha kazi hiyo ili kuepuka makazi holela na kubainisha kuwa ucheleweshaji wowote utasababisha mji kutopangika na kusisitiza lazima isimamiwe kwa umakini.

Sambamba na hilo, Dk. Mabula alisema wilaya ya Mkuranga bado hajafanikiwa katika upimaji pamoja na kuwa na viwanda vingi na kushauri wakati wa upimaji lazima halmashauri iainishe pia maeneo ya uwekezaji.

Naye Mbunge wa Mkuranga ambaye pia ni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema Mkuranga ina viwanda vingi kutokana kuwa na eneo linalovutia na kuongeza kuwa atafurahi kama Wizara ya Ardhi itafanya jitihada za kuharakisha urasimishaji.

"Kama serikali itaongeza kasi kidogo ya kupanga na kurasimisha maeneo ya wilaya hii basi itakusanya kiasi kikubwa cha fedha maana Mkuranga imekuwa lango na ni kimbilio la wananchi kutoka Dar es Salaam kutokana na mkoa huo kujaa na mahali pekee pa kupumulia ni Mkuranga," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Mhandisi Mshamu Munde, alisema halmashauri yake ina migogoro mingi ya adhi ya kurithi na wapo katika kukabiliana changamoto za ardhi ikiwemo makazi holela.

Kutokana na changamoto hizo, alisema tayari kuna kampuni saba zinazofanya kazi ya urasimishaji na kusisitiza kuwa mkakati wa halmashauri yake ni kuzuia uanzishwaji makazi holela.

# Waziri Mkuu kombole Ikungi kwa usimamizi fedha za umma

**Na Elisante John,** SINGIDA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa ameipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida kwa matumizi sahihi ya fedha za umma kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Aidha, ameziagiza halmashauri zingine nchini kuiga mfano wa matumizi bora ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wananchi.

Akizungumza na watumishi wa Halmashauri za Wilaya ya Manyoni, Itigi, watumishi wa sekretarieti ya mkoa na kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa huo, katika siku ya kwanza ya ziara yake mkoani Singida jana, Majaliwa alisema kwa ujumla utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye halmashauri hiyo unaridhisha.

Waziri Mkuu alisema katika kuhakikisha fedha za umma zinatumika kikamilifu, watendaji na madiwani wanatakiwa kusimamia vyema matumizi yake kwa kufuata miongozo, kanuni na taratibu kama zinavyotakiwa.

Alisema wananchi wanatarajia kunufaika kupitia miradi ya maendeleo ambayo inakwenda kutatua kero zao na kwamba ni wajibu wa watumishi waliopewa jukumu kuwajibika.

Pia alisema serikali haitasita kuchukua hatua dhidi ya mtendaji yeyote atakayeshindwa kuwajibika na kujihusisha na matumizi mabaya ya fedha za umma.

Waziri Mkuu alitembelea mradi kubwa wa maji wa Kintinku-Lusilile wilayani Manyoni, utakaogharimu zaidi ya Sh. bilioni 10 hadi utakapokamilika na ukitarajiwa kuhudumia zaidi ya watu 55,000 katika kata nne za halmashauri hiyo.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, aliishukuru serikali kwa kupeleka fedha nyingi za maendeleo zaidi ya Sh. Bilioni 388 kwa ajili ya miradi mbalimbali ikiwamo elimu, afya na maji.

HABARI KITAIFA

# Chadema yaonya makatibu siri za chama

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimewaonya makatibu wa majimbo ya Simiyu, Mara na Shinyanga kutoa nje siri za chama hicho.

Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji, alisema hayo juzi alipokuwa akikabidhi Kompyuta 12 kwa makatibu wa majimbo hayo, zilizotolewa na Mbunge wa Viti Maalumu mkoani Simiyu, Gimbi Masaba, kwa ajili ya kuhifadhia taarifa za chama kwa mfumo wa kidijitali.

Alisema kutokana na makatibu wa majimbo hayo kupewa kompyuta hizo, hivyo hatarajii kusikia siri za chama zikiwa zimevuja nje kwa sababu utunzaji wake utakuwa salama zaidi tofauti na awali ulivyokuwa kwa mfumo wa makaratasi.

"Dunia ya sasa inaondokana na kutunza taarifa kwa kutumia makaratasi bali tunakwenda kwa mfumo wa kidijitali, hivyo kompyuta hizi zitumieni vizuri pamoja na kutunza siri za chama, kwa sababu uhifadhi wa taarifa zenu utakuwa salama zaidi," alisema Mashinji.

Naye Masaba, ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Serengeti inayounganisha mikoa ya Mara, Simiyu na Shinyanga, alisema ameguswa kutoa kompyuta hizo ili siri za chama zibaki kuwa salama tofauti na awali.

Alisema siri za chama hazikuwa katika hali ya usalama kutokana na makatibu wa majimbo kuhifadhi kwenye mfumo wa makaratasi pamoja na kwenda kuzichapa kwenye komputa za watu binafsi ambazo si sahihi kiusalama.

Katibu wa Jimbo la Simiyu, Charles Malimi, kwa niaba ya wenzake, alipongeza kupewa kompyuta hizo na kubainisha zitawasaidia kuhifadhi taarifa zao kiusalama zaidi na kutunza siri za chama.

Malimi alikiri dhahiri kuwa awali siri za chama hazikuwa salama kutokana na kutumia mfumo wa kizamani wa analojia.



Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Vincent Mashinji akizungumza na makatibu wa majimbo wa chama hicho, kutoka Simiyu, Mara, na Shinyanga juzi, baada ya kumaliza kupewa mafunzo kuhusu matumizi ya kompyuta kwa ajili ya kuhifadhia taarifa za chama kwa mfumo wa kidijitali. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Watalii 1,000 Israel kutua nchini

**Na Elizabeth Zaya**

ZAIDI ya watalii 1,000 kutoka Israeli wanatarajia kuwasili nchini mwezi huu kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) na Zanziba kwa ajili ya shughuli za kitalii.

Watalii hao wanatarajiwa kuwasilia katika makundi matatu kuanzia leo, wengine Octoba 12 na 13, mwaka huu.

Hii ni mara ya pili kwa watalii kwa idadi hiyo kutoka nchini humo, baada ya Aprili mwaka huu kuwasili kupitia KIA kwa ndege tatu tofauti.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Bodi ya TTB, Jaji mstaafu Thomas Mihayo, alisema watalii hao wanatarajia kutembelea Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Hifadhi za Taifa za Serengeti, Tarangile na Zanzibar. "Sekta ya utalii Tanzania imefunguka rasmi. Tunaona idadi kubwa ya watalii wameanza kuelewa vivutio tulivyo navyo na wameanza kumiminika. Oktoba ni mwezi wa neema sana kwetu kwa sababu unakuwa na idadi kubwa ya wataalii," alisema Jaji Mihayo.

"Tunaamini kwamba hata amani tuliyo nayo Tanzania inachangia watalii kuongezeka. Bila hivyo sidhani kama wangemiminika hivi hata kama tungekuwa na vivutio vizuri namna gani," aliongeza.

Mwenyekiti huyo alisema ni wakati mwafaka pia kwa Watanzania husussani katika maeneo ambayo yanatembelewa na watalii hao kuchangamkia fursa za kibiashara. "Unajua Tanzania ndiyo kwanza soko linafunguka. TTB tumefanya kazi kubwa ya kutembea katika nchi mbalimbali kutangaza vivutio tulivyo navyo na sasa tunaona dunia imeanza kuvielewa," alisema na kuongeza:

"Ni wakati na sisi Watanzania kuchangamkia fursa mbalimbali, tuhakikishe wanapokuja wanatuachia pesa nyingi kwa hiyo tutengeneze bidhaa ambazo wakiziona lazima wanunue na fursa nyinginezo za kibiashara."

# BoT wachangia ujenzi wa vyoo

**Na Hamisi Nasiri,** MTWARA

WAFANYAKAZI wa Benki Kuu ya Tanzania (Bot) Tawi la Mtwara, wamechangia fedha zao binafsi Sh. milioni 2.4 kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo mkoani hapa.

Fedha hizo zilitolewa juzi na Kaimu Mkurugenzi wa Tawi hilo, Mussa Mzia, kwa niaba ya wafanyakazi wenzake.

Mzia alisema wameguswa na kampeni hiyo ya 'Shule ni Choo' ambayo imeanzishwa na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, kutokana na dhamira yake ya kuboresha sekta ya elimu.

Alisema BoT Tawi la Mtwara, inatambua umuhimu wa huduma ya vyoo bora shuleni, hivyo shule ikiwa na choo bora uwezekano wa wanafunzi kufanya vizuri kitaaluma ni mkubwa.

Mzia alisema mazingira bora ya shule ikiwamo miundombinu ya matundu ya vyoo ni jambo la msingi na la umuhimu na kuongeza kuwa BoT siku zote imekuwa ikithamini jamii na kuwa mstari wa mbele katika kushirikiana kutatua changamoto zilizopo.

"Sisi wafanyakazi wa BoT Tawi la Mtwara kwa pamoja tunachangia kampeni hii ya Shule ni Choo kwa kila mmoja wetu kutoa kile alicho nacho. Kwa ujumla tumepata Sh. milioni 2.4 hivyo tunakabidhi," alisema Mzia.

Alisema Benki Kuu inafanya kazi katika jamii na imezungukwa na taasisi mbalimbali, hivyo ni lazima iunge mkono jitihaza zozote zinazolenga kutatua changamoto hizo.

Mzia pia alisema wafanyakazi wa BoT bado wanaendelea kutafakari kuona namna gani pia watasaidia katika maeneo mengine ya kijamii.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Byakanwa, aliwashukuru wafanyakazi hao kwa kitendo cha kusaidia kampeni ya Shule ni Choo.

"Nashukuru sana kwa kusaidia hili na kuguswa hadi kuamua kuja hapa kutoa kiasi hiki cha fedha. Najua fedha hizi zimetoka mifukoni mwa wafanyakazi wenyewe na si ofisi ya Benki Kuu," alisema Byakanwa.

Mkuu wa Mkoa alisema jamii kwa ujumla iachane na utamaduni wa kuchangia sherehe mbalimbali kama vile harusi na badala yake ichangie kutatua changamoto zilizopo katika jamii.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunawatakia mafanikio wanariadha wetu, U-20

**KWA** mara nyingine bendera ya Tanzania kupitia yosso wa Tanzania Bara inatarajiwa kupeperushwa katika fainali ya mashindano ya soka ya vijana wa umri chini ya miaka 20 (U-20) ya Afrika Mashariki na Kati itakayochezwa leo katika mji wa Jinja nchini Uganda.

Timu hiyo ya Tanzania Bara itashuka dimbani kuwakabili wapinzani wao Kenya katika fainali hizo za mashindano hayo yanayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa).

Yosso hao wa Tanzania Bara watakutana na wenzao hao wa Kenya wakiwa hawajapoteza mchezo hata mmoja kuanzia mechi za hatua ya makundi, lakini ikiwa na kumbukumbu ya kutoka sare ya mabao 2-2 na majirani zao.

Inaelezwa kuwa, kikosi hicho kinachoongozwa na Mzalendo Zuberi Katwila ndio timu ambayo imelelewa kwa muda mrefu, wachezaji wake wengi wakiwa ni waliopandishwa kutoka katika kikosi cha Tanzania kilichoshiriki fainali za vijana ya umri chini ya miaka za Afrika (Afcon 2019).

Ni timu ambayo imepata uzoefu wa kucheza mashindano na mechi mbalimbali za kitaifa na kimataifa.

Gazeti hili tunawaombea dua na mafanikio wachezaji wa timu hiyo ili wakamilishe kazi waliyoianza na hatimaye kurejea nyumbani na kikombe cha mashindano hayo.

Kunyakua ubingwa wa mashindano hayo, si tu kutaipa sifa Tanzania, pia kutawaweka wachezaji hao sokoni kwa klabu mbalimbali za ndani na nje ya nchi kuwafuatilia kwa lengo la kuwasajili na hapo itakuwa ndio mwanzo wa kujipatia kipato kupitia vipaji vyao.

Huu ni wakati muhimu kwa nyota wa Tanzania kuweka historia ya kushinda kikombe hicho, na vile vile kutakiwa kujiandaa kujiunga na timu nyingine za Taifa ikiwamo ile ya U-23 na Taifa Stars.

Wanachotakiwa kukifanya yosso hao wa Tanzania Bara, ni kushuka uwanjani ikiwaheshimu wapinzani wao, kwa sababu nao wataingia kwenye mchezo huo kwa lengo la kuibuka mabingwa.

Nipashe inawakumbusha yosso wa Tanzania na benchi lao la ufundi kuwa, hakuna fainali mbili, wanatakiwa kupambana kuhakikisha wanapata matokeo chanya katika mchezo huo na kuwapa furaha Watanzania ambao wana kiu ya kuona timu zao za hapa nchini zinatwaa mataji mbalimbali.

Nipashe pia inapenda kuwatakia kila la kheri wanariadha watatu wa hapa nchini ambao leo usiku wanatarajiwa kupeperusha bendera ya Tanzania katika mashindano ya riadha ya dunia yanayofanyika katika mji wa Doha, Qatar.

Bendera ya Tanzania katika mashindano hayo itapeperushwa na Alphonce Simbu, Augustino Sulle na Stephano Huche, ambao wote watachuana katika mbio za kilomita 42 (marathoni).

Licha ya kuwapo kwa changamoto ya hali ya joto kali ambayo ilimfanya mwanariadha wa kike, Failuna Abdi, kushindwa kumaliza mbio hizo, bado Watanzania wana imani na nyie, baada ya kufanya maandalizi mazuri kabla ya kuondoka nchini na kwenda kushiriki mbio hizo za dunia.

Hakuna jambo gumu kila mahali kwenye nia, kama iliwezekana kwa Simbu kutwaa medali kwenye mbio za Mumbai Marathon, hata leo pia wanariadha wote wa Tanzania wanaweza kufanya vizuri katika mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Riadha la Kimataifa (IAAF).

Tunaungana na wadau wote wa michezo nchini kuwatakia kila la kheri yosso wa U-20 pamoja na wanariadha ambao wanalitumikia taifa huko Qatar.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Tuondokane na aibu hii

**'AIBU'** ni jambo la kumvunjia mtu heshima; jambo la kumtia mtu fedheha; tahayuri, soni. 'Aibika' ni shikwa na aibu baada ya kufanya jambo la kufedhehesha, pata aibu, fedheheka.

Mpira wa miguu, yaani kabumbu, kandanda au soka ni mchezo upendwao sana duniani. Hapa nchini, timu zenye wanachama na mashabiki wengi zaidi ni Yanga iliyoanzishwa mwaka 1936 ikifuatiwa na Simba mwaka 1935.

Ndizo timu zilizotwaa ubingwa wa Ligi Kuu nchini mara nyingi, Yanga ikiizidi Simba kwa kutwaa mara nyingi zaidi na sasa wakijiita 'mabingwa wa kihistoria.'

Mashindano ya kimataifa, Simba ilifanya vizuri zaidi hata kufikia fainali ya Kombe la Washindi Afrika ingawa ilifungwa 2-0 na Stella Abidjan ya Ivory Coast mwaka 1993 kwenye Uwanja wa Taifa ambao sasa waitwa Uwanja wa Uhuru.

Hata hivyo Simba imekuwa ikizipa shida timu za Waarabu kwa kuzifunga ndani na nje kwenye michuano ya kimataifa. Wanapopangwa kupambana na Simba, hujizatiti sana, tofauti na wanapopangwa na Yanga.

Ingawa Yanga ilianzishwa mwaka mmoja kabla ya Simba, haijafikia hatua iliyofikia Simba kucheza fainali ya Kombe la Afrika. Ilichofanya ni kuishia robo fainali tu katika kuwania Kombe hilo maarufu la vilabu Afrika.

Kuteleza si kuanguka. Mtu aweza kuteleza asianguke. Methali hii hutumika kumnasihi mtu aliyekumbwa na matatizo asikate tamaa bali aendelee. Huweza pia kutumiwa na mtu aliyekumbwa na shida kuwajuza wenzake kuwa hajakata tamaa au bado ana ujasiri wa kuendelea kupambana.

Huenda timu zetu hushindwa kutokana na tabia ya kuamini zaidi ushirikina (tabia ya kuamini uwezo wa kiumbe kingine/chengine juu yako badala ya ule wa Mwenyezi Mungu)! Kadhia (tukio la kuhuzunisha) hii imefikia hata wachezaji kurogana wenyewe kwa wenyewe ili kujitafutia umaarufu!

Niwazindue viongozi na wachezaji wa timu zetu za kandanda: "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili yako yote."

"Mimi ni BWANA Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa. Usiwe na miungu mingine ila mimi. Usijifanyie sanamu ya kuchonga, mfano wa kitu chochote kilicho juu mbinguni, au kilicho chini duniani, au kilicho majini chini ya nchi. Usivisujudie wala kuvitumikia.

Imeandikwa: "Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu Yeye peke yake. Mche Bwana Mungu Wako: Ndiye Peke Yake Utakayemtumikia."

Yawezekana kutenda dhambi dhidi ya mapendo ya Mungu kwa namna mbalimbali:

*Upurukushani: huzembea au hukataa kujali upendo wa Mungu; kushindwa kutambua uzuri unaoendana nao na kuikataa nguvu yake.

*Utovu wa shukrani: hushindwa na kukataa kukiri mapendo ya Mungu na kumrudishia pendo kwa pendo.

*Utepetevu: ni kusita au kuzembea kujibu mapendo ya Mungu. Unaweza kuwa ni pamoja na kukataa kujitoa kwa msukumo wa upendo.

*Uzembe au uvivu wa kiroho hususia wema wa Mungu.

*Chuki ya Mungu hutokana na kiburi. Ni kinyume cha mapendo ya Mungu ambaye wema wake inaukataa, na ambaye inamdhania kuwa huapiza kama mmoja anayekataza dhambi tu na kutoa adhabu. (Rejea Katekisimu ya Kanisa Katoliki Uk. 470:2093-94).

Wewe mcheza kandanda unayekwenda kwa mchawi ili 'aisafishe nyota yako' kwa kumroga mchezaji mwenzako ili aporomoke nawe utwae nafasi yake, uliumbwa na mchawi au Mungu?

Huyo mchawi alijiumba mwenyewe au Mungu yule yule aliyekuumba wewe? Unapomkana Mungu hapa duniani, kiyama (siku ambayo ulimwengu na kila vilivyomo vitafikia mwisho na wafu watafufuliwa, watasimamishwa mbele ya Mola wao kwa ajili ya kuhesabiwa na kulipwa kwa matendo yao duniani) utakuwa mgeni wa nani?

Ni wajibu wa viongozi wa klabu na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kukaa pamoja na kutafuta mbinu zitakazozipa mafanikio klabu hizo na Timu za Taifa katika mechi zake za ndani za za kimataifa badala ya kutegemea uchawi. Vinginevyo tutaendelea kuwa 'vichwa vya wendawazimu' na 'majamvi ya wageni!'

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

HABARI KITAIFA

# Waziri asisitiza matumizi ya kiberenge Mlima K'manjaro

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amesema mpango wa matumizi ya kiberenge au magari maalum ya kutumia nyaya atika Mlima Kilimanjaro uko pale pale.

Amesema lengo la kutumia magari hayo ni kuongeza idadi ya watalii wanaopanda mlima huo kutoka 50,000 hadi milioni moja kwa mwaka.

Kwa mujibu wa takwimu, idadi kubwa ya watalii wanaoingia nchini ni wazee na wamekuwa wakikosa fursa hiyo ya kupanda mlima huo kutokana na umri wao.

Akizungumza baada ya kupokea watu maarufu wakiwamo wasanii walioongozwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, baada ya kuteremka katika mlima huo kupitia geti la Marangu katika Kampeni ya "Twen'zetu Kileleni" iliyoasisiwa na waziri huyo, Kanyasu alisema suala la matumizi ya kiberenge katika mlima huo haliepukiki.

Kanyasu aliwatoa wasiwasi wapagazi na waongoza watalii wanaofanya kazi katika mlima huo kuwa matumizi ya kiberenge hicho hayataathiri kazi zao badala yake itaongeza ajira maradufu.

Alifafanua kuwa kiberenge hicho hakitatumika katika njia za miguu zinazotumika kupanda mlima huo kwa sasa na badala yake kitatumika katika maeneo tofauti.

Kanyasu pia alisema kiberenge hicho kitakuwa kikitumiwa na wazee, watoto, watu wenye ulemavu na watafiti mbalimbali na si kwa watalii wanaofika kupanda kwa ajili ya kufurahia 'adventures'.

Aliongeza kuwa utalii wa kutumia kiberenge si kitu kigeni duniani kwa kuwa umekuwa ukifanyika Sweden, Vietnam na Russia kwa ajili ya kuwawezesha watalii wasio na uwezo wa kupanda milima nao kufika kileleni.

Waziri Kigwangalla, ambaye ni waziri wa kwanza katika wizara hiyo kupanda mlima huo hadi kileleni, alisema matumizi ya kiberenge katika mlima huo yanahitaji mjadala wa kitaifa na anajipanga kukutana na makundi mbalimbali kwa ajili ya majadiliano hayo.

Hata hivyo, alisema mabadiliko yanapotokea huwa na faida pamoja na hasara lakini kwa mabadiliko hayo ya matumizi ya kiberenge, kuna faida zaidi kuliko hasara kwa serikali na wadau wa utalii kwa ujumla.

Katika hatua nyingine, Waziri Kigwangalla aliutaka uongozi wa Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro kuzifanyia kazi baadhi ya changamoto alizoziona katika mlima huo hasa malazi kwenye baadhi vituo.



Mkandarasi akiendelea na ujenzi wa Barabara ya Igesa, eneo la Sinza Makaburini, jijini Dar es Salam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kampeni ya usajili simu yawagusa Chalinze

**Na Mwandishi Wetu,**
CHALINZE

WAKAZI wa Chalinze na maeneo ya jirani, wamejitokeza kwa wingi katika kampeni ya mnada kwa mnada kwa ajili ya kusajili laini za simu kwa alama za vidole inayoendeshwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Kwenye usajili huo, TCRA inashirikiana na kampuni za simu, Jeshi la Polisi Kitengo cha Uhalifu Mitandaoni, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) na Idara ya Uhamiaji.

Kampeni hiyo tangu imeanzishwa imefanywa katika mikoa 15 lengo likiwa nchi nzima kufikiwa na wananchi kusajili simu zao.

Mkuu wa TCRA Kanda ya Mashariki, Mhandisi Lawi Odiero, alisema ni fursa kwa wananchi wa Chalinze na viunga vyake kusajili laini za simu kwa alama za vidole na huduma nyinginezo kutokana na kuwapo kwa mnyororo wadau wa mawasiliano.

Mhandisi Odiero alisema kampeni ya mnada kwa mnada inayoendeshwa na TCRA ilianzishwa ili kutoa fursa ya wananchi kuhudumiwa hasa wakati huu usajili wa laini za simu kwa alama za vidole.

Alisema muda uliopo ni miezi mitatu hivyo wananchi wakamilishe taarifa zinazohitajika katika kujisajili laini za simu kwa alama za vidole.

Aidha, alisema kampeni hiyo inalenga kuimarisha ulinzi katika mawasiliano ya simu pamoja kufanya mawasiliano kuwa salama katika nchi.

Odiero alisema kampeni hiyo ni kwa ajili ya kutoa elimu ya mawasiliano kwa kushirikiana na wadau katika kujibu changamoto wanazokutanazo katika utumiaji wa mawasiliano nchini.

Mkuu huyo alisema wananchi wasio na vitambulisho vya Nida wahakikishe wanapata na usajili wa laini za simu kwa kutumia alama za vidole na huduma nyinginezo za mawasiliano hayo.

Kanda ya Mashariki itapita katika wilaya zote katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Lindi Mtwara.

Alisema kuna watu wengine wanatumia mawasiliano ya simu bila kujua na kwamba Jeshi la Polisi lipo katika kampeni ya mnada kwa mnada ili kuwaelewesha makosa ya jinai yatokanayo na matumizi ya simu.

Pia alisema kampeni hiyo ni endelevu katika kuwafikia wananchi ili kuhakikisha kila mmoja anasajili laini yake kwa alama za vidole kwa kutumia kitambulisho cha taifa.

Naye Ofisa Mawasiliano Mwandamizi wa TCRA, Mabel Masasi, alisema mwitikio umekuwa mkubwa kwa wananchi kutaka vitambulisho kwa ajili ya kusajili laini za simu kwa alama za vidole.

Masasi aliwataka wananchi watumie fursa hiyo kupata elimu na baada ya kuisha mnada sehemu husika waende katika mamlaka husika kupata vitambulisho.

Aliongeza kuwa watahakikisha kila mwananchi anasajili kwa alama za vidole kwa kuwa watu wana haki ya kuwa na mawasiliano ya simu.

# Mdau wa elimu ampongeza JPM

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

UONGOZI wa shule zinazomilikiwa na kampuni ya MHL, umempongeza Rais John Magufuli kwa uwekezaji katika miradi mikubwa ya kimaendeleo pamoja na uchapaji kazi wake.

Pia Rais amepongezwa kwa kuziboresha shule kongwe katika miundombinu, ikiwamo kuziboresha shule za kata ambapo kwa sasa zinafanya vizuri katika mitihani ya kidato cha nne na cha sita.

Mkurugenzi Mtendaji wa MHL, inayomiliki shule za St. Mathew's, Victory, St.Mark's na Ujenzi, Peter Mutembei, alitoa pongezi hizo juzi wakati wa mahafali ya kidato cha nne ya shule hizo.

"Uongozi wa shule unampongeza Rais Magufuli kwa uchapakazi wake. Kwa sasa kila Mtanzania ameona miradi mikubwa ya maendeleo inavyofunguliwa, ikiwamo kuboreshwa kwa shule kongwe na shule za kata," alisema.

Mutembei alisema kuanzishwa kwa shule za kata kumewasaidia wanafunzi wengi kupata elimu tofauti na zamani walipokuwa wakipata nafasi hiyo vijana wachache.

Akizungumzia mafanikio na matokeo mazuri katika shule za MHL, alisema nidhamu iliyopo kwa walimu na wanafunzi imekuwa kila mwaka ikichochea hali ya ufaulu.

Kwa mujibu wa Mutembei, zaidi ya watoto 600 wanatarajia kufanya mitihani ya kidato cha nne mwezi ujao.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tamisemi), Mwita Waitara, aliyekuwa mgeni rasmi katika mahafali hayo, alisema serikali inatambua mchango unaotolewa na shule binafsi.

Waitara alisema serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa shule binafsi kutokana na mchango mkubwa wa elimu ambao zinautoa.

Pia alizitaka shule binafsi kuwaangalia watoto wenye uhitaji kwa kuwapatia elimu bure katika shule zao.

"Wapo watoto wenye uhitaji, hawana uwezo wa kuendelea na masomo kwa sababu ya kipato. Shule binafsi mkiwachukuwa watoto watano watano mtakuwa mnapunguza idadi ya uhitaji kwa watoto hao.

# Mwili wa mwanafunzi wenye deni mil. 26/- hospitalini waruhusiwa

INATOKA UK. 3

akizungumza na gazeti hili jana , alisema mtoto wao alifariki dunia Septemba 30 mwaka huu, lakini walikwama kuchukua mwili wake huo kutokana na kudaiwa gharama za matibabu ambazo zilikuwa nyingi na hawakuwa na uwezo wa kulipa.

Alisema hali hiyo iliwapa wakati mgumu na kuwafanya wahahe kwenda ustawi wa jamii ili kupata msamaha na kuruhusiwa kuchukua mwili huo kwa ajili ya maziko.

"Mwanaidi alihamishiwa kwenye hospitali ya Mloganzila ikiwa ni rufaa kutoka Hospitali ya Amana Julai 5 mwaka huu, ametibiwa hapo hadi alipofariki deni likawa limefikia kiwango hicho ambacho ndugu tulishindwa kumudu kulipa," alisema.

Mkembe ambaye ni mkazi wa Saranga, wilayani Ubungo, ambako msiba unafanyika, alisema walihangaika kwenda kujieleza kwa viongozi ndipo wakashauriwa kwenda ustawi wa jamii ili kupata msamaha.

"Hatimaye leo (jana) tumefanikiwa kupata mwili huku deni likipunguzwa hadi kufikia Sh. milioni tano ambazo tumetakiwa tuzilipe kwa awamu, " alisema Mkembe.

Shangazi huyo alibainisha kuwa Mwanaidi alikuwa akisumbuliwa na miguu kuishiwa nguvu hadi akapooza na walikuwa wakimuuguza kulingana na uwezo walio nao.

Ofisa Uhusiano wa Hospitali hiyo, Neema Mwangomo, alipoulizwa kuhusiana na jambo hilo aliahidi kulifuatilia katika kitengo husika na kutolea taarifa.

Matukio ya miili kuzuiwa hospitalini kutokana na ndugu kushindwa kumudu gharama za matibabu, yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara kiasi cha miili mingine kukaa kwa muda mrefu huku gharama zikiongezeka.

Agosti 11, mwaka huu, Rahel Kitwai, aliamua kumweleza Rais John Magufuli amsaidie ,baada ya mwili wa mama yake kuzuiwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) kutokana na kutolipiwa gharama za matibabu za Sh. milioni tano.

Mama huyo baada ya kumwona Rais Magufuli anapita hospitalini hapo, alipaza sauti kuomba amsaidie kwa kuwa mwili wa mama yake ulizuiwa na ndipo Rais alipolipa deni hilo na mama huyo kuruhusiwa kuchukua mwili huo.



Katibu wa Hamasa na Chipukizi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Ilala, Fadiga Legele, akizungumza na vijana wa chama hicho pamoja na wanachama katika ufunguzi wa Kisukuru ya Kijani iliyofanyika katika Mtaa wa Mianzini, Ilala , jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA**

# JPM apongeza bakora za RC

INATOKA UK. 2

wote 392 wa kidato cha tano na sita katika Shule ya Sekondari Kiwanja ikiwa siku moja baada ya kuwacharaza viboko wanafunzi 14 wa shule hiyo kwa kosa la kumiliki simu za mkononi.

Licha ya kuwarejesha nyumbani, aliwaamuru wanafunzi hao kulipa Sh. 200,000 kila mmoja kwa wanafunzi 366 huku wenzao 26 waliokamatwa na simu za mkononi kulipa Sh. 500,000 kila mmoja kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili ya shule ambayo yalichomwa moto.

Akizungumza na wanafunzi hao jana, Chalamila aliwapatia saa nne kufungasha kila kilicho chao na kuondoka shuleni hapo huku akiwataka kurejea Oktoba 18, mwaka huu wakiwa tayari wamelipa fedha hizo kupitia akaunti ya shule.

Wanafunzi 26 ambao walikamatwa na simu, licha ya kulipa Sh. 500,000 kila mmoja siku ya kurejea shuleni, anatakiwa kufika na mzazi huku wengine 366 kila mmoja akitakiwa kuandika barua ya kukiri na kuahidi kutorudia makosa kama hayo shuleni hapo. "Tunafunga kidato cha tano na sita kwa sababu hamna mahali pa kulala. Mabweni mliyokuwa mkilala ndiyo mmeyachoma moto, hivyo kuanzia sasa mnaondoka kwenda kwa wazazi wenu na mtarudi hapa Oktoba 18," alisema Chalamila.

Alisisitiza kuwa wanafunzi wote wanatakiwa kurejea shuleni kila mmoja akiwa amelipa kiasi hicho cha fedha huku akionya kuwa yeyote atakayekaidi serikali itamfuata huko aliko na kumkamata.

"Usipolipa fedha hizo kabla ya Oktoba 18 na ukaacha kuripoti shuleni, tutakufuata huko huko uliko kwa pingu na kuanzia sasa hakuna uhamisho wa wanafunzi shuleni hapa," alisema.

Chalamila alisema hata kama mwanafunzi ambaye hatalipa fedha hizo akihamia shule binafsi, atafuatwa huko na kuzuiwa kufanya mtihani wa taifa wa kidato cha sita popote ndani ya mipaka ya Tanzania.

Alisema walimu waliokuwa wakifundisha kidato cha sita pia wanapewa mapumziko kwa kipindi hicho ambacho wanafunzi watakuwa nyumbani.

Endapo wanafunzi wote 366 watalipa kila mmoja Sh. 200,000 kama walivyoamuriwa Sh. milioni 73.2 zitapatikana na wale 26 kila mmoja akilipa Sh. 500,000 kama walivyoamuriwa, Sh. milioni 13 zitapatikana, hivyo kufanya kiwango cha fedha hizo kuwa Sh. milioni 86.2.

Septemba 30, mwaka huu, mabweni ya Shule ya Sekondari Kiwanja yaliteketea kwa moto, tukio ambalo linahusishwa na wanafunzi ambao siku hiyo hiyo mchana, walipekuliwa na kunyang'anywa simu na walimu wao.

# Watuhumiwa 50wajitokeza kulipa wasamehewe makosa

INATOKA UK. 3

Arusha, Hakimu Mkazi Rose Ngoka, alisema mahakama inawatia hatiani washtakiwa hao baada ya kukiri mashtaka yanayowakabili.

Watuhumiwa waliokuwa wakikabiliwa na kesi na kukiri makosa yao ni Josephat Shayo (41) ambaye ni dereva na mkazi wa Olasiti, Latifa Mwarengwa (33) mkazi wa Kisongo na Bakari Kunga (46) mkazi wa Njiro.

Hakimu Ngoka alisema mahakama imejiridhisha kuwa walikutwa na madini ya aina nane ambayo ni tanzanite, sapphire, spinel, ruby, tourmaline, tsavorite, grossular na aquamarine ambayo walikuwa wakiyatorosha kwenda nchini Kenya.

Alisema kutokana na kosa hilo, wanatiwa hatiani na kuamuru mshtakiwa wa kwanza (Shayo) na wa pili (Latifa) waliokabiliwa na makosa tisa ya kujimilikisha madini na kusafirisha bila kuwa na vibali, kila mmoja kulipa faini ya Sh. milioni 45 au kwenda jela miaka mitatu kila mmoja.

Katika kosa la 11 alisema linawakabili washitakiwa wote watatu ambapo aliamuru (Shayo kulipa faini ya Sh. milioni tano, Latifa pia faini kama hiyo au jela miaka mitatu.

Alisema mshtakiwa wa tatu, Kunga, anahukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni 10 au jela miezi mitatu na pia Sh.milioni 100 ya fidia ya kukwepa kulipa kodi mbalimbali za serikali, ikiwemo kodi ya mrabaha ifikapo jana.

Hakimu Ngoka alisema fedha zingine Sh. milioni 100 watatakiwa kulipa ndani ya siku saba kuanzia hukumu zilipotolewa.

Alisema sambamba na hilo, Mahakama imeamuru kutaifisha madini kilo 31.59 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 416,577.58 sawa na Sh. milioni 958 na gari namba T.645 DBY aina ya Suzuki Swift rangi ya bluu nyeusi.

"Washitakiwa watakapolipa fidia na faini hizo ndipo waachiwe huru. Kabla ya hapo watakaa mahabusu,"alisema

Kabla ya hukumu hiyo kutolewa Wakili Mkuu wa Serikali Martenus Marandu, aliwasilisha hati mbili kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) ya kuwapa mamlaka mahakama hiyo kusikiliza kesi hiyo namba 59/2019 ya uhujumu uchumi.

Pia alidai DPP amewaondolea kosa la utakatishaji fedha lililokuwa linawakabili washitakiwa hao na kuomba mahakama kujielekeza kwenye kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili.

Aliomba mahakama hiyo itoe adhabu inayostahili na kuwataka washitakiwa walipa fidia kwa kuisababishia hasara serikali kwa kukwepa kodi.

**Imeandikwa na Hellen Mwango (DAR) na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**.

# Wafanyakazi OBC wakubali yaishe

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

HAKIMU Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Arusha, Rose Ngoka, juzi aliwahukumu washtakiwa 10 ambao ni raia wa kigeni, kulipa Sh. milioni 100 au kwenda jela miezi 12 kwa kosa kufanya kazi bila kibali.

Raia hao wa kigeni walikuwa wakifanya kazi katika kampuni ya uwindaji ya Oterlo Businness Coperation (OBC) kinyume cha sheria. Waliohukumiwa adhabu hiyo ni Darweshi Jumma, Riaz Aziz Khan, Mohammad Tayyab, Ali Bakhash, Abdulrahman Mohammed, Martin Crasta, Imtiaz Feyaz, Arshad Muhammad, Hamza Sharif na Zulfiqar Ali.

Hakimu Ngoka alisema mahakama imewatia hatiani washtakiwa hao kwa kukiri kufanya kosa hilo nchini na kuamuru kila mmoja kulipa faini ya Sh. milioni 10 au kwenda jela miezi 12.

"Lakini kwa kuzingatia maombi ya wakili wenu wa utetezi, Steven Mosha na kwa kuangalia mazingira ya kesi na madhara ya kijamii kama alivyosema, mahakama imewakuta na hatia, hivyo itawapa adhabu hiyo ili iwe fundisho kwa wengine," alisema.

Mbali na kuwapa adhabu ya kulipa faini, pia aliwaonya washtakiwa kutii sheria, kanuni na taratibu za nchi pindi wanapoingia nchini.

Wakili wa utetezi, Mosha, kabla ya hukumu hiyo kutolewa, aliomba mahakama kuwapa adhabu ndogo washtakiwa kwa sababu ni kosa lao la kwanza kufanya.

"Hakimu naomba mahakama iwapunguzie adhabu kwa sababu wamekiri na kuokoa muda wa mahakama. Lakini pia washtakiwa wawili wana utaifa wa nchi ya India na wanane raia wa Pakistan na walishtakiwa miezi mingi nyuma na walitumia gharama kubwa kuishi," alidai.

Kutokana na kushtakiwa, alidai kuwa walilazimika kutumia fedha nyingi kuishi nchini na wengi wao ni vijana wanahitajika kwenda kulijenga taifa lao.

"Mheshimiwa Hakimu naomba uwape adhabu ndogo kwa sababu wengine umri wao ni mkubwa wanahitaji kukaa wana familia zao," alidai.

Aidha alidai kuwa kuwapa adhabu kubwa kutasababisha ugumu wa maisha kwa familia zao, hivyo aliomba wapewe adhabu ya kulipa fedha kwa sababu wako tayari kulipa kiasi chochote ambacho mahakama itaamuru.

Kabla ya wakili wa utetezi kutoa maombi hayo, Wakili Mkuu wa Serikali Maritenus Marandu, alidai kuwa kabla ya jana washtakiwa hao, waliandika barua iliyowasilishwa na wakili ikionyesha washtakiwa hao kukiri makosa yao.

Pia aliiambia mahakamani hiyo kuwa upande wa Jamuhuri hauna kumbukumbu za makosa ya nyuma lakini aliomba mahakama iwape adhabu inayostahili kulingana na kosa walilofa




Mlezi wa wanafunzi wa Chuo cha St. Joseph, Mathew Ngulugulu (kushoto), akiwapa zawadi ya maua wanafunzi wa uhandisi wa chuo hicho, waliowasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam juzi, wakitokea nchini India walikokuwa wakisomea fani hiyo kwa ufadhili wa chuo hicho. Kutoka kulia ni Penina Angolo, Sonia Sillas na Modester Ndelwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waomba kusitishwa mbegu zilizoboreshwa

**Na Allan Isack,** BABATI

WAKULIMA mkoani Manyara wameiomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo kusitisha mpango wa matumizi ya mbegu zilizobadilishwa vinasaba ili kuwaepusha kuwa tegemezi wa mbegu kutoka nje ya nchi.

Wakulima hao waliyasema hayo juzi mjini hapa kwenye mkutano mkuu wa Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (Mviwata), ukiwa na kauli mbiu ya mtetezi wa mkulima ni mkulima mwenyewe.

Kwa mujibu wa wakulima hao, teknolojia hiyo inayotumika kubadilisha vinasaba vya mbegu bado haiko nchini hivyo ni tatizo kubwa kwa wakulima.

Lohay Langai, mmoja wa wakulima hao, alisema mbegu hizo zilizobadilishwa vinasaba (GMO) huenda zisiwe na tija kwa wakulima kulingana na mazingira na hali ya hewa ya maeneo mengi nchini.

Langai alisema hali hiyo itasababisha wakulima kuwa tegemezi wa mbegu kutoka nje ya nchi na kuchelewesha upatikanaji na inaweza kuwa moja ya sababu zitakazoporomosha uchumi wa wakulima.

Mwenyekiti wa Mviwata Mkoani Manyara, Mohammed Hussein, alisema alidhani serikali imewaletea mbegu hizo wakulima kwa lengo la kuboresha kilimo, lakini kumbe zimekuwa zikiwafanya wakulima waendelee kuwa tegemezi.

# Mwenyeki Longido achaguliwa ALAT

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Sabore Molloimet, amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Tawala za Mikoa (ALAT) Mkoa wa Arusha.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo uliofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa halmashauri ya Arusha DC, Makamu Mwenyekitiwa ALAT Mkoa wa Arusha, Kalisti Lazaro, alisema uchaguzi huo umefanyika kwa mujibu wa kanuni za kudumu za mikutano ya uchaguzi wa viongozi wa jumuiya za mwaka 2009, kifungu cha 42, 43 na 44.

Kalisti ambaye ni Meya wa Jiji la Arusha, alisema Molloimet amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa ALAT Mkoa wa Arusha bada ya kupata kura za ndio zaidi ya nusu kutoka wajumbe waliooshiriki mkutano huo. Alisema Molloimet alipata kura 21 za ndio kati ya kura 22 zilizopigwa na wajumbe huku kura moja ikiharibika. Atakuwa katika nafasi hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Akizungumza baada ya kuchaguliwa, Molloimet aliwashukuru wajumbe kwa kumpa dhamana ya kushika nafasi hiyo na kuwaomba washirikiane kufanya kazi na waweke pembeni tofauti zao za kiitikadi kwa maslahi mapana ya wananchi waliowachagua na taifa kwa ujumla.

Molloimet aliahidi kutumia uwezo alionao kusimamia nafasi hiyo kwa haki na huku akiwataka wajumbe kutimiza wajibu wao na kuheshimu makubaliano na kusimamia utekelezaji wake.

"Nashukuru kwa kunipa nafasi hii na uwezo ninao. Naahidi kuutumia kwa kutenda haki na zaidi tutumie nafasi zetu kuwahudumia wananchi kwa maslahi ya wananchi," alisema.

Mwenyekiti huyo anachukua nafasi hiyo iliyoachwa wazi na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Karatu, Jubilete Mnyenye, aliyepoteza sifa za kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo.





## Wafugaji wateka soko la maziwa

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

WAFUGAJI wa ng'ombe wa maziwa wa mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara wameanza kunufaika na soko uhakika la maziwa, baada ya serikali kupiga marufuku uingizwaji wa maziwa kutoka nje ya nchi.

Jana, wafugaji hao wa Kanda ya Kaskazini wa ng'ombe wa maziwa katika kata ya Mwika Kaskazini, Wilaya ya Moshi, walimweleza Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, kuwa marufuku hiyo imekuwa na matokeo chanya.

Walimweleza kuwa imewezesha mazao ya mifugo yao kupanda thamani na kuchochea ongezeko la kipato chao.

Prof. Ole Gabriel alikwenda katika eneo hilo kutembelea wafugaji wa ng'ombe waliopo kwenye mradi wa uboreshaji wa vinasaba vya ng'ombe wa maziwa nchini pamoja na kukagua kiwanda cha kusindika maziwa cha Kondiki.

Katika risala yao kwa Katibu Mkuu , Meneja wa kiwanda cha Kondiki, Peter Odero, alisema kwa sasa, soko la maziwa ni la uhakika na kwamba changamoto kubwa ni magonjwa na vifungashio vya maziwa.

"Tatizo hivi sasa liko katika vifungashio ambavyo ni maalum kwa ajili ya kusafirisha kupeleka kwenye masoko ya nje ya Mkoa wa Kilimanjaro. Kutokana na hali hiyo, tunalazimika kuagiza vifungashio kwa gharama kubwa nchi jirani ya Kenya,"alieleza Odero

Akizungumza baada ya kauli hiyo ya wananchi, Prof. Ole Gabriel alisema lengo la wizara yake ni kuwasaidia wafugaji kufuga kisasa na kwamba kwa sasa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inafanya majadiliano na Wizara ya Kilimo kuhakikisha kila mazao ya mifugo kuanzia manyoya na kinyesi vinakuwa na thamani.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TAWIRI), Eligy Shirima, alimweleza Prof. Ole Gabriel kuwa tayari wameingia katika makubaliano na kampuni ya uendeshaji wa ranchi za taifa (Narco) kwa ajili ya kutenga maeneo ya malisho.

Wilaya ya Siha peke yake, ina mbuga yenye ekari zaidi ya 3,500 za malisho ya mifugo na inamilikiwa na Narco.

# Viberenge kubeba watalii K'manjaro

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAZIRI wa Maliasili na Utalii Dk. Hamisi Kigwangalla, amemaliza ubishi matumizi ya kiberenge au magari ya kutumia nyaya za umeme, kubeba watalii katika Mlima Kilimanjaro.

Aidha, ameahidi kuwa utalii huo utaanzishwa wakati wowote kwani hauna madhara. Kigwangalla aliyasema hayo jana, baada ya kuweka rekodi ya kuwa Waziri wa Utalii kufika kilele cha Uhuru cha Mlima Kilimanjaro chenye urefu wa mita 5,895 kutoka usawa wa bahari.

Alisema hayo alipozungumza na wadau mbalimbali waliojitokeza kushiriki kampeni maalum ya 'Kili Challenge 2019, Twenzetu Kileleni'. Kampeni hiyo inalenga kuwahamasisha Watanzania kuupigia kura kwa wingi mlima huo ili ushinde na kutangazwa kuwa kivutio bora cha utalii duniani.

Kigwangalla alisisitiza hakuna madhara yanayoweza kutokea hususani kupoteza ajira za wapagazi na kuharibu mazingira.

Mjadala huo uliibuliwa tena wiki iliyopita na Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira wakati akizindua kampeni hiyo, baada ya kutaka Waziri wa Maliasili na Utalii kuhitimisha ndoto hiyo au kuruhusu mjadala wa kitaifa.

Alisema wapo watalii watakaopanda mlima huo kwa kupitia njia ya miguu na wapo watakaopanda kwa viberenge, na kwamba utalii wa kiberenge unatumika sehemu mbalimbali duniani.

Alisema faida za kupanda mlima huo kwa kiberenge ni kubwa kwani huwazesha watalii wengi kupanda Mlima Kilimanjaro kwa wakati mmoja wakiwamo wazee,watoto na wenye ulemavu wataweza kupanda mlima huo.

"Kuna kundi kubwa la watalii wazee ambao hawawezi kupanda mlima kutokana na umri wao lakini hawa wataweza kuja kupanda mlima Kilimanjaro endapo kutakuwepo na huduma ya kiberenge" alisema Dk.Kigwangalla Alisema kiberenge pia kinatumika kufanya uokozi wa watalii wanaoshindwa kupanda mlima huo kutokana na sababu mbali mbali za kimazingira na afya. Alisema utalii ni chimbiko la uhakika wa mapato ya serikali na kutoa wito kwa Watanzania kupenda uzalendo kwa Taifa lao na kutembelea hifadhi za taifa ili kuweza kuimarisha mapato ya nchi.

Tanzania inataka kuongeza idadi ya watalii kupitia magari ya kutumia nyaya katika hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ambao ni mrefu zaidi Afrika. Akizungumza juzi, wakati akizindua kampeni maalum ya kuupigia kura mlima huo, Mghwira alisema:

"Ninaamini pia kwamba, baada ya tukio hili la Kili Challenge 2019, Twenzetu Kileleni, Waziri utatusaidia kuhitimisha na kuongoza mjadala wa matumizi ya kiberenge katika Mlima Kilimanjaro, kama unakuja ama hauji ama unafaa au haufai,"alieleza Mghwira

Awali kulikuwa na taarifa kwamba, tayari serikali ilikuwa imeanza mazungumzo na kampuni moja ya China na nyinginezo kutekeleza mradi huo.

Njia iliyokuwa inapendekezwa kutumika kwa kiberenge hicho cha utalii ni ile ya Machame ambayo kwa mujibu wa watoa huduma, ndio inayopitisha wageni zaidi kuliko nyingine zote kuelekea mlimani. Kiberenge hicho kinatajwa kwamba kinaweza kuongeza idadi ya watalii kwa asilimia 50, kwa sababu kina uwezo wa kuwawezesha wale wasioweza kupanda mlima huo kwa miguu kufika kilele cha Uhuru chenye urefu wa mita 5, 895 (kilometa 5.8).

Aina hiyo ya kuchochea utalii haitakuwa ya mara ya kwanza duniani, kwa vile magari ya kutumia nyaya au viberenge yapo nchini Sweden, Italia na Himalaya.

Kwa sasa, Mlima Kilimanjaro unawania tuzo ya dunia ya kivutio bora cha utalii kinachoongoza kwa mwaka 2019. Kilimanjaro pamoja na nchi nyingine duniani zinazosifika kwa utalii, zimeorodheshwa na taasisi ya kimataifa ya World Travel Awards 2019 na kuingizwa katika shindano hilo.




Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu (wa pili kulia), akimkabidhi cheti cha hongera, Msanii wa kwanza wa filamu, Kulwa Kikumba maarufu kwa jina la Dude, baada ya kufanikiwa kufika kileleni katika Mlima Kilimanjaro kupitia kampeni ya "Twenzetu Kileleni", iliyoasisiwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla (wa tatu kushoto), katika hafla iliyofanyika juzi. **PICHA: WMU**

# Watalii kufurika 'Swahili Festival'

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

TANZANIA inatarajia kupokea mawakala wa utalii kutoka katika nchi 200 duniani wakati wowote kuanzia sasa.

Mawakala hao wanakuja nchini kushiriki Tamasha la Swahili litakalofanyika katikati ya mwezi huu.

Kwa nyakati tofauti katika mahojiano maalum na Nipashe, Mkurugenzi wa Bodi ya Utalii nchini (TTB) Devotha Mdachi na Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Jaji mstaafu Thomas Mihayo wamethibitisha ujio wa wageni hao.

Mahojiano hayo yalifanyika wakati wa kuwapokea watalii 17 kutoka nchini Uingereza wakiwamo waendesha teksi wa jijini la London ambao waliwasili mkoani Kilimanjaro, kwa ajili ya kupanda Mlima Kilimanjaro.

Kwa mujibu wa mkurugenzi wa bodi hiyo, pia serikali itapokea kundi jingine kubwa la watalii 200 kutoka nchi ya Israel ambao wanakuja kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii hapa nchini.

"Hao watalii na mawakala wanakuja Tanzania baada ya kupata hamasa kubwa kutokana na juhudi kubwa zinazofanywa na TTB, kwa kushirikiana na mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania nje ya nchi, wakifanya kazi kubwa ya kuitangaza pamoja na utalii wake,"alisema Mdachi

Alieleza kuwa kundi la madereva wa teksi wa London walikuja nchini kupanda Mlima Kilimanjaro ili kuchangisha fedha kwa ajili ya kuwaenzi wanajeshi mashujaa ambao wamestaafu pamoja na kupunguza uzito wa miili.

Madereva wa teksi hao walipanda Mlima Kilimanjaro kupitia lango la Lemosho, Wilaya ya Siha na baadaye kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Aidha, bodi hiyo imeeleza kuwa kwa mwaka jana, TTB kwa kushirikiana na kampuni binafsi zinazofanya biashara za utalii ndani na nje ya nchi na kwamba watalii milioni 1.5 walifika Tanzania.

Pia, alisema kwa mwaka huu, juhudi za kutangaza utalii zimeongezeka na kwamba wanategemea kupokea watalii 2,000,000 watakaotembelea vivutio mbalimbali vya utalii hapa nchini.

Baadhi ya watalii hao ambao ni madereva teksi akiwamo Brign Heffrnan, wameeleza furaha yao ya kufika kwa mara ya kwanza nchini Tanzania kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

Kilele cha uhuru cha Mlima Kilimanjaro, kina urefu wa mita 5,895 takribani kilometa 5.8 sawa na futi 19,340 ndicho kivutio kikubwa kinachopendwa na wageni wengi kutokana na kufunikwa na theluji katika nchi ya joto. Ni kivutio ambacho ni nadra.







Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Deus Seif (kushoto), akimkabidhi Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, msaada wa mifuko 300 ya saruji kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa miundombinu ya sekta ya elimu jijini humo, jana. Kulia ni Mwenyekiti wa CWT wa mkoa huo, Samwel Mkotya. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanaume vinara unywaji pombe

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa kati ya Watanzania watatu, mmoja anatumia pombe huku wanaume wakiongoza kwa unywaji.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alisema juzi kuwa takwimu za utumiaji pombe kupita kiasi kwa mwaka zinaonyesha wanaume wanatumia pombe lita 32.7 kulinganisha na wanawake ambao wanatumia lita 12.6.

Alisema kwa takwimu hizo, inaonyesha wanaume ndio vinara wa utumiaji wa pombe ambao umepitiliza.

Aidha, alisema asilimia 30 ya Watanzania wenye umri wa miaka 15-56 wanatumia pombe hali ambayo inakwamisha shughuli mbalimbali za maendeleo.

"Takwimu za watumiaji pombe zinaonyesha kati ya Watanzania watatu mmoja anatumia pombe jambo ambalo si zuri," alisema.

"Matumizi ya pombe za kienyeji zinazotengenezwa kwa nafaka ndizo zinazoongoza kuwa na watumiaji wengi na kusababisha uhaba wa chakula. Asilimia 86 ya watumiaji wa pombe wanatumia pombe ya kienyeji na asilimia iliyobaki inatumia pombe kali, bia na mvinyo," aliongeza.

Dk. Ndugulile alisema kwa takwimu hizo ni dhahiri jamii inapata udumavu kutokana na lishe duni kwa kuwa nafaka nyingi huelekezwa katika matumizi ya pombe za kienyeji.

Alisema serikali itaendelea kurekebisha sheria na kanuni za matumizi ya bidhaa za pombe nchini ili kupunguza madhara yanayowapata watumiaji.

Katibu Mkuu wa Mtandao wa Kupinga Unywaji Pombe (TAAnet), Gladness Munuo, aliyataja baadhi ya madhara ya unywaji pombe kupita kiasi kuwa ni pamoja na magonjwa ya afya ya akili, moyo, figo, ini na mishipa ya fahamu.

Munuo aliongeza kuwa wakiwa wadau na watetezi wa taifa wanaopinga matumizi ya pombe, wanafanya kila jitihada kuhakikisha jamii inabaki kuwa salama na

# Waziri Mkuu ahimiza kupiga kura

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewataka wananchi wenye sifa ya kupiga kura kujitokeza kujiandikisha kwa kuwa ni haki yao ya msingi.

Majaliwa alitoa kauli hiyo juzi zikiwa zimesalia siku nne kuanza uandikishaji wa wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 24, mwaka huu, alipokuwa akifungua mkutano wa sita wa mwaka wa tathmini ya masuala ya lishe nchini. Uandikishaji huo utaanza Oktoba 8 hadi 14, mwaka huu, nchini kote na uzinduzi wake utashuhudiwa na Rais John Magufuli mkoani Katavi. Waziri Mkuu alisema nchi itaingia kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, hivyo watu wote wana haki ya msingi ya kuchagua na kuchaguliwa.

"Wito kwa Watanzania wenye sifa ya kujiandikisha katika orodha ya wapiga kura kuchukua fomu kugombea nafasi mbalimbali na kushiriki kupiga kura kwa kuwa ni haki yenu kikatiba," alisema.

Kuhusu uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura, Majaliwa alisema wanaotakiwa kujiandikisha ni wale wote ambao wamepoteza vitambulisho vyao au vimeharibika. "Wengine ni wale ambao wamehama kutoka sehemu moja kwenda nyingine, wale waliofikisha miaka 18 lakini hawana kadi ya kupigia kura, wanafunzi wenye miaka 17 kwa sasa lakini ifikapo mwaka 2020 Oktoba watakuwa na miaka 18," alisema.

Hata hivyo, alitaka elimu itolewe kwa watu wanaotakiwa kujiandikisha na kuchagua viongozi watakaoweza kuongoza kwa uadilifu.

Hivi karibuni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alisema Watanzania milioni 26.9 wenye sifa za kupiga kura, wanatarajiwa kuandikishwa kwa ajili ya uchaguzi huo.

Alisema uandikishaji utafanyika kuanzia Oktoba 8 hadi 14, mwaka huu na idadi ya wanaume wanakadiriwa kuwa 12,852,328 huku wanawake ni 14,108,157 .

"Kukata rufani dhidi ya uamuzi wa pingamizi itakuwa Oktoba 21-23 na uamuzi wa rufani ni Oktoba 21-26,"alisema Alisema kukoma kwa viongozi waliopo madarakani ni Oktoba 22, kuchukua fomu za kugombea Oktoba 29 na kurejesha ni Oktoba 29 hadi Novemba 4.

"Uteuzi wa kamati za rufani Oktoba 29, uteuzi wa wagombea Novemba 5, uwasilishaji wa mapingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea Novemba 5-9, uamuzi wa pingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea Novemba 5-7, kukata rufani kuhusu pingamizi la uteuzi Novemba 5-9," alisema.

Kuhusu ratiba ya kampeni, uwasilishaji wa ratiba wa mikutano ya kampeni kutoka kwenye vyama vya siasa Novemba 10, uwasilishaji wa ratiba kwa mkuu wa polisi wilaya Novemba 14, kuanza kwa kampeni Novemba 17-23 na uchaguzi rasmi ni Novemba 24.

# CWT yatoa mifuko 300 saruji Dodoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) kimetoa msaada wa mifuko 300 ya saruji kwa jiji la Dodoma ili kusaidia kukabiliana na uhaba wa vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na matundu ya vyoo.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya kukabidhi msaada huo, Ofisa Elimu Msingi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mabeyo, alisema msaada huo umekuja wakati mwafaka kutokana na changamoto nyingi katika maeneo mbalimbali kwa namna tofauti.

Mabeyo alisema katika eneo la vyumba vya madarasa, mahitaji ni vyumba 2,438 wakati vilivyopo ni 916 ikiwa upungufu ni 1,522.

Alisema changamoto nyingine ni uhaba wa walimu kwa kuwa mahitaji halisi ni 2,438 wakati waliopo ni 1,777, hivyo kufanya kuwa na upungufu wa walimu 661.

"Kwa upande wa nyumba za walimu, alisema mahitaji ni 1,777 na nyumba zilizopo ni 167. Kutokana na hali hiyo, alisema upugufu ni nyumba 1,610. Madawati mahitaji ni 32,509 na yaliyopo 25,496 ikiwa pungufu ni madawati 7,013", alifafanua Mabeyo.

Pia alisema changamoto nyingine ya miundombinu katika jiji hilo ni vyoo ambapo hivi sasa mahitaji kwa wavulana ni matundu 1,936 yaliyopo 509, pungufu ni 1,427.

"Kwa wasichana mahitaji ni matundu 2,456 na vilivyopo ni 577, ambapo pingufu ni matundu 1879" alibainisha Mabeyo.

Akikabidhi mifuko hiyo, Katibu Mkuu wa CWT, Deus Seif, alisema lengo la msaada huo ni kushirikiana na walimu katika kutimiza wajibu.

Alisema wakiwa chama cha walimu nchi, hawana budi kuhakikisha miundombinu inayotumiwa na walimu na wanafunzi kuwa katika mazingira mazuri.

"Kama walimu watakuwa na nyumba bora katika maeneo ya jirani na maeneo yao ya kufundishia lazima watafanya kazi kwa tija lakini pia kwa wanafunzi kama watakuwa na matundu ya vyoo ya kutosha watakipokea kile wanachofundishwa vizuri," alisema Seif.






Meneja Mkazi wa Equinor Tanzania, Dk. Mette Halvorsen Ottoy (kushoto), akizungumza wakati wa kongamano la mafuta na gesi, lililomalizika jijini Dar es Salaam juzi, na kushirikisha nchi 67 duniani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Hospitali yanasa muuguzi feki

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

HOSPITALI ya Mnazimmoja mjini Zanzibar, imemnasa 'mfanyakazi feki' aliyekuwa anajifanya muuguzi, licha ya kwamba si mtaalamu, alikuwa akihudumia wagonjwa katika wodi ya wazazi .

Mwanamke huyo mwenye miaka 21 anadaiwa kuwa si muuguzi, wala hana taaluma hiyo na si mwajiriwa wa hospitali hiyo.

Msichana huyo, aliyetambulishwa kwa jina la Fatma Muhamed Abdallah, mkazi wa Magogoni Zanzibar, amedaiwa kuwa alikuwa akitoa huduma hospitalini hapo kwa muda wa siku nne mfululizo bila ya kugundulika kuwa sio mfanyakazi wa hospitali hiyo. Akizungumza na wanahabari msichana huyo alisema ameamua kufanya kazi hiyo ya kutoa huduma hospitalini hapo kwa sababu anaipenda kazi hiyo ingawa hajaisomea.

Alisema kuwa amemaliza kidato cha sita mwaka jana lakini ameshindwa kwenda chuoni kusomea fani hiyo kwa sababu hana uwezo wa kifedha.

"Kazi ya uuguzi na udaktari naipenda na wala hapa sijaja kwa nia mbaya,"alisema.

Msichana huyo alikuwa akitoa huduma katika wodi ya wazazi na kugundulika kuwa si mfanyakazi baada ya kutoka na mtoto nje ya wodi wakati sio utaratibu.

Riziki Ramimu Suheri, mlinzi katika kitengo cha wazazi hospitalini hapo, alisema kuwa walimgundua msichana huyo kuwa si mfanyakazi kutokana na vituko ambavyo aliokua akivifanya ambavyo ni kinyume na utaratibu .

Alieleza kuwa msichana huyo huvaa mavazi rasmi ya wauguzi na wakati mwingine hujivalisha kama daktari na hutoa huduma mbalimbali katika wodi ya wazazi.

Abubakari Khamis Hamad, Mkurugenzi wa Utawala na Uendeshaji wa Hospitali ya Mnazi mmoja, alisema tukio hilo ni la kihalifu kwa sababu muuguzi huyo hana taaluma yoyote ya kutibu.

Alieleza kuwa walimfuatilia msichana huyo na kugundua kuwa si mfanyakazi wa hospitali hiyo na hivi sasa yupo chini ya ulinzi na uchunguzi wa polisi.

Alieleza kuwa mbali ya tukio hilo mwanzoni mwa mwaka huu walimkamata mtu mmoja ambaye alijifanya mgonjwa hospitalini hapo kumbe alikua

# Pweza, ngisi, kamba hatarini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI imeeleza jinsi uharibifu wa mazingira unavyosababisha samaki jamii ya ngizi , pweza na kamba kuanza kupungua.

Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ametoa angalizo na onyo hilo jana wakati akijibu swali kwenye kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Dk.Makame Ali Ussi, alisema kuna samaki wa aina mbalimbali ambao wamepungua wakiwamo pweza, ngisi na kamba kutokana na kuvunjwa kwa matumbawe ambayo ni sehemu za mazalia yao.

''Tumeanza kuziona athari za uharibifu wa matumbawe. Baadhi ya samaki wameanza kuadimika kama pweza kutokana na kuvunja matumbawe','alisema Naibu Waziri.

Ussi alionya kuhusu uvuvi haramu unaofanywa na watu wenye tamaa kuwa umechangia kuharibika kwa mazalia ya samaki au matumbawe.

Aliwakumbusha wavuvi kwamba zipo sheria zinazokataza uvuvi haramu na kueleza adhabu yake kuwa mvuvi atakayetiwa hatiani ikiwa amevua samaki wachanga atalazimika kulipa faini ya Sh.10,000 na haitazidi 1,000,000 au kifungo cha miezi mitatu jela.

"Mheshimiwa sheria za uvuvi zitapambana na wavuvi wanaoendesha uvuvi haramu unaohatarisha matumbawe na samaki kwa ujumla"alisema Ussi.

Waziri Ussi alikuwa akijibu swali la mwakilishi wa jimbo la Mgogoni, Shehe Hamad Matar, aliyetaka kufahamu athari za uvuvi haramu na taarifa za hali ilivyo hadi sasa ikiwamo katika maeneo ya hifadhi za viumbe bahari.

Alisema uvuvi haramu na nyavu za kukokota pamoja na baruti umechangia kuharibika kwa matumbawe kufuatia wavuvi kuyavunja wanapolipua maeneo hayo.

Aidha, alisema uvuvi wa kutumia jamii za majani ili kuwalewesha samaki maarufu kama utupa, nao umekuwa chanzo kingine cha kuharibu matumbawe.

Alieleza kuwa kwa mujibu wa sheria ya uvuvi namba saba ya mwaka 2010 kifungu cha 22 kinakataza uvuvi haramu wa aina zote ikiwamo nyavu za kukokota pamoja na mitego.

Alisema athari za uvuvi haramu zinazotikisa ni pamoja na kupungua kwa kiwango kikubwa cha samaki katika maeneo ya majini ya kawaida yanayofikiwa na wavuvi wengi wa kawaida.

# Snida yapewa jukumu viwanda

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Viwanda imesema kuwapo kwa wakala wa kuendeleza viwanda vidogo (Snida) ndiyo ukombozi wa kuwawezesha wazalishaji wadogo kupiga hatua kimaendeleo.

Naibu Waziri Hassan Khamis Hafidh, alisema hayo wakati akitoa ufafanuzi kuhusu malengo ya wakala ya Snida.

Alisema malengo ya wakala wa kuendeleza viwanda vidogo ni kusaidia wafanyabiashara wadogo na wazalishaji wa bidhaa mbali mbali kupiga hatua na kujiongezea kipato.

Aliwataka wazalishaji wa bidhaa mbali mbali kujitokeza kwa wingi kujiunga na Snida kwa ajili ya kuendeleza shughuli za biashara.

Alizitaka faida zinazopatikana kupitia wakala wa viwanda vidogo kuwa ni pamoja na mafunzo mbalimbali ya ujasiriamali, fedha za mkopo za kuwaendeleza wajasiriamali wadogo na taarifa za masoko na fursa mbalimbali.


''Mkombozi wa wafanyabiashara wadogo ni Snida ambayo wazalishaji wa bidhaa mbali mbali wanatakiwa kujiunga ili kupata mbinu na mipango ya kuendeleza biashara hizo','alisema Hafidh.



**MWANA FA** Soma UK.16

JUMAMOSI OKTOBA 5, 2019

BT BURUDANI TELE




# UPWEKE

## BEN POL AMPA MTIHANI ANERLISA

Soma UK.14

BASI SAWA



## Mwana FA, Dude waonesha uzalendo

HUU ni uzalendo wa nguvu! Pengine unaweza kuona jambo la kawaida, lakini kwa wasanii Mwana FA na Dude wanaona kumaliza upandaji wa Mlima Kilimanjaro sawa na kuonesha uzalendo.

Wasanii hao walifanikiwa kufika kilele cha mlima kati ya wasanii 30 waliojitokeza kupanda Mlima Kilimanjaro kwenye kampeni ya Twenzetu Kilimanjaro iliyoandaliwa na Waziri wa Utalii na Maliasili, Dkt. Hamisi Kigwangalla.

Wakizungumza baada ya kushuka walisema wamefurahia kufika kileleni na hilo linawapa faraja kwa kuona jambo hilo sawa na uzalendo wa hali ya juu dhidi ya nchi yao.



# UPWEKE
## BEN POL AMPA MTIHANI ANERLISA

MWANAMUZIKI wa miondoko ya taratibu, Ben Pol, amethibitisha kutaka kuwa karibu na mke wake mtarajiwa Anerlisa Muigai ili kuondokana na upweke.

Hivi karibuni Anerlisa ambaye ni raia wa Kenya, aliandika ujumbe katika ukurasa wake wa Instagram akisema mpenzi wake huyo anataka ahamie Tanzania ili kuiimarisha ndoa yake.

Hata hivyo mrembo huyo alisema bado anaonyesha shaka kuhusu suala hilo.

"Suala la kumtaka mke wako si baya, mnapokuwa wawili na kubadilishana mawazo mnajenga mambo mengi na mimi nataka iwe hivyo," amesema Ben Pol.



## Mpoto amleta Nyerere karibu

BINGWA wa mashairi, Mrisho Mpoto, amemtaja Mwalimu Julius Nyerere kama kiongozi wa kipekee kutokea duniani kutokana na kujali utu na maadili.

Akizungumza hivi karibuni, amesema kamwe hawezi kujutia kumuimba na kumtukuza kutokana na matendo mema.


"Huwezi kumuacha kiongozi kama huyu bila ya kumuimba au kumtukuza, mimi nimeamua kufanya shoo maalum pale Makumbusho kwa ajili yake," amesema Mpoto.

INSTA-TWITTER






**Nimekosa** cha kuandika jamani nisaidieni-**Nandy.**



**Usiniambie** walichokisema kuhusu mimi, bali niambie kwa nini walijisikia huru kwako kunisema vibaya mimi mbele yako?-**Johari.**



# Kala sifa jipe mwenyewe

RAPA mkali Kala Jeremiah, amelishauri Baraza la Sanaa Tanzania(Basata) kuwa na utaratibu wa kuwapongeza wasanii wanaoimba nyimbo zinazoelimisha jamii.

Amesema yeye ni mmoja wa wanamuziki waliojitolea kuelimisha, lakini chombo hicho hakijatambua kazi zake licha ya makamu wa rais Samia Suluhu Hassan kumpongeza.

"Mimi nashauri viongozi wa Basata watambue kazi zetu zinazoelimisha, badala ya kuzifuangia nyimbo na kuwapa promo za bure wasanii," anesema Kala




**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**



# P THE MC MAWENGE AKAMILISHA ALBAM

WAKATI wasanii wakubwa wanasuasua kwa kutoa singo moja, rapa P The Mc Mawenge, amekwenda mbali baada ya kuachia Albam yake ya kwanza yenye nyimbo 12.

Albam huyo inayoitwa "CLEO" ilianza kuwa sokoni mwishoni mwa wiki hii.

"Kukamilisha albam hii mpya nataka kuonesha mabadiliko katika fani ya muziki, lazima tufikirie mbali kuliko kutoa singo ambayo huwezi kunufaika nayo," amesema.

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Kukataliwa** na wengine kwa sababu hawaamini kama unaweza kufanya jambo lolote kubwa ni moja ya mtihani mikubwa kwenye safari ya maisha. Ni lazima ujiandae kuushinda. Usikubali wakukatishe tamaa na kusitisha ndoto zako, hakuna mwenye mamlaka ya maisha yetu zaidi ya Mungu-**Jenifer Kyaka Odama.**



**Hivi** baba zetu waliweza vipi kujenga majumba, maana mimi kila nikipata hela nasikia harufu ya mishikaki tu-**Ibrajim Ajibu.**



**Mimi** ni mpole, masikini mpaka najionea huruma. Ila baba yangu atanipa mume wa kufanana nae mwenye upendo wa kweli kama nilivyo mimi-**Kabula.**

# Kuumbe!

## WABONGO WANALETA NYODO WAMAREKANI WANAFURAHIA FURSA



WANAMUZIKI wa Bongo ukiwaambia Tanzania kuna maeneo mazuri yanayofaa kuchukulia picha za video zao watakuona kama mtu uliyechanganyikiwa.

Wao hawaamini kama mazingira ya hapa Bongo yanaweza kumpaisha na kufanya video ya nyimbo zao kuonekana bora na inayovutia.

Kutokana na kasumba hiyo, wasanii wengi wanatumia pesa nyingi kwa ajili ya kugharimia safari ya kwenda nje nchi za nje hasa Afrika Kusini na Ulaya kwa ajili ya kazi hiyo.

Tabia hiyo imezidi kuota mizizi kiasi kwamba utawasikia baadhi ya wasanii wakijigamba kwamba wao video zao ni za hali ya juu eti picha za video zao zina mandhari ya nje.

Hata hivyo, mwanamuziki wa Marekani mwenye asili ya Morocco French Montana, amewaumbua wasanii hao malimbukeni baada ya kuaamua kwenda Uganda na kuchukua picha ya wimbo wake katika mazingira duni.

Video ya wimbo wake huo uitwao Unforgettable aliyomshirikisha Swae Lee, umepata umaarufu kiasi ambacho katika mtandao wa You yube inaongozwa kwa kutazamwa na watu wengi katika muda mfupi.

Video hiyo imepata mrejesho mzuri kutoka sehemu zote za duniani, na kuwafanya French Montana na muongozaji wa video hiyo kutajwa kama watu wenye jicho la kipekee kuona fursa hiyo.

Mpaka jana video hiyo imetazamwa na watu bilioni moja jambo ambalo limevunja kabisa ile kasumba kwamba mazingira ya nchi za Afrika Mashariki machafu na hayafai kwa kuboresha video za wasanii wa muziki.



## Nandy, Vanessa sikilizeni Makumbele

**Na Adam Fungamwango**

MAGEUZI ya muziki wa kizazi kipya, yaliwaingiza akinadada wengi kwenye tasnia ya muziki.

Hii ni tofauti na zamani ambapo kulikuwa na waimbaji wachache sana wa kike kama kina Rahma Shally, Emma Mkelo, Nana Njige, Kida Waziri na wengineo.

Kwa sasa kuna wasanii wengi wa kike si kwenye muziki wa dansi tu, bali hata kwenye bongo fleva ambako ndiko wamejaa zaidi. Hata hivyo bado wasanii jao wana mapungufu machache hasa kwenye utunzi. Idadi kubwa ya wasanii wa kike wanaimba mapenzi. Haikatazwi, lakini wanatakiwa nyimbo zao kubeba hisia za matatizo ya kike yanayotokea kwenye jamii yetu.

Labda wanadhani nyimbo za aina hizo hazitapendwa, lakini si kweli kwani matatizo wanayoyapata wanawake miaka 100 iliyopita, hadi leo ni yaleyale.

Wasanii wa kike wa sasa hasa wanaotamba ni Nandy, Maua Sama, Vanessa Mdee na wengine.

Leo tutazame baadhi ya nyimbo zinazoeleza matatizo wanayoyapata wanawake ndani ya jamii, lakini zikitungwa na wanaume na kuuwasilisha ujumbe kwenye jamii ili kuelimisha, kurekebisha, kukosoa na kuonya.

**Mnanionyesha Njia ya Kwetu-DDC Mlimani Park**

Ni wimbo unaomuonyesha mjane akilalamika baada ya kufiwa na mumewe. Anawachana ndugu wa mume kuwa baada ya mumewe kufariki, wameanza kumuonyesha mlango wa kutokea kabla hata matanga hayajaisha na pia wameanza kugawana mali ya marehemu mumewe.

Mama anawaambia hivi wanasahau kuwa mali hiyo ni ya watoto na yeye mama yao. Anawashangaa ndugu hao kumkana leo, wakati mumewe akiwa hai walimheshimu, wakimwita shemeji, mkewe, wifi lakini yote leo yamewasahau. Wimbo huu ni wa katikati ya miaka ya '80 ukitungwa na Cosmas Thobias Chidumule ambaye kwa sasa ameokoka.

**Jiko Limenuna-Vijana Jazz Band**

Wimbo huu ni wa mwanzoni mwa miaka ya '80, ukitungwa na Hemed Maneti akiwa na Vijana Jazz Band.

Mwanamke amekutana na shemeji yake, anamwambia amsaidie kwani mume wake haonekani mwezi mzima sasa nyumbani, watoto wanalia njaa. Hana pesa, hana kitu nyumbani, yeye mwenye hajala pia. Anamwambia kama kuolewa mambo yenyewe ni hivyo bora tu arudishwe kwa wazazi wake akatulie.

Mama anasema angekuwa peke yake angefanya uamuzi wa kujinyonga, lakini moyo wake ni kwa watoto.

**Ndoa ya Mateso-Majirani Rajab**

Marijani Rajabu naye hakuwa nyuma, alitunga wimbo ambao unamzungumzia mama mmoja ambaye matatizo yake ya ndoa yalimfika shingoni na kuamua kuyapeleka kwa mjumbe.

Anamwambia mjumbe jinsi mwanamume alimvyomtoa nyumbani kwao kwa vigelegele na heshima nyingi, lakini sasa amemgeuka, halali nyumbani, haachi pesa nyumbani, badala yake anashinda baa.

Mjumbe anamtuliza na kusema kuwa ataongea naye ili kumaliza tatizo hilo.

**Nyumba imenishinda-Juwata Jazz Band**

Huu ni wimbo wa miaka ya katikati ya '70, na ulitungwa na Hassan Rehani Bitchuka.

Ni mwanamke anayemwambia mumewe amrudishe kwao kwa sababu nyumba imeshinda.

Tatizo lililopo, anamwambia haelewani na watoto waliowakuta kwenye nyumba hiyo, kwani kila akiwatuma au kuelekeza jambo wao wanamchukulia kama ni mama wa kambo.

Anamwambia amechoka kwa sababu haoni sababu ya kutukanwa na watoto hao, badala yake anamwambia amrudie mama yao ili walee watoto.

**Makumbele-Maquiz Original**

Ni wimbo wa miaka ya mwishoni mwa '80. Ulitungwa na Kaumba Kalemba akiwa na Maquiz Original.

Unamzungumzia mama ambaye amevumilia mengi kwa baba watoto wake Makumbele, lakini sasa amefika mwisho, anamwambia atarudi kwa baba na mama yake, mawazo yake yote yatakuwa kwa watoto wake, lakini pia mazoea ya mapenzi yatamtesa, ingawa hata hivyo atajitahidi ili ayasahau kwa sababu amepata mateso makubwa kwenye ndoa hiyo.



# Vijimambo

1. Wanasema eti mimi chizi. Watanzania bwana kwa figisu! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Duuh! Jamani kazi kwanza, kuselifika baadae - Bahati, Kiwalani DSM.
3. Hii mitandao ya kijamii inatutesa. Kwa hii selfii kila mtu atakomenti 'nice' - Agatha Mbale, Moro Town.
4. Natafuta picha ya kutupia 'whatsap' - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
5. Kijana hiyo simu imepitwa na wakati, ipeleke makumbusho - Oiso, Nyaishozi Tegeta DSM.
6. Ukisikia uchizi taslimu, basi ndio huo. Simu ya mezani na selfii! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.
8. Yes, hapa sasa pozi limekubali, ngoja nijifotoe sasa - Samwel Sungi, Utemini Singida.
9. Hii simu vipi, mbona sioni sehemu ya kujiselfisha? - Msabaha J. Msabaha, Mikindani Mtwara.
10. Lazima baby wangu aikubali hii picha, si selfii ya kitoto - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Hii inaitwa 'ekotite', muulizeni Kofi Olomide anaifahamu sana - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
12. Kweli ushamba mzigo. Wewe, sio kila simu unaweza kujiselfisha nayo - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
13. Ha ha haaa, usitake ncheke mie! Hebu rudisha simu ya watu ofisini - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Hapo 'chacha'! Disco limeingia watu wa kabila lileee! Mtajuta kuijua selfii - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
15. Mnashangaa nini? Mie sijiselfishi kama nyie, mie fundi simu jamani - Dully, Kiembesamaki Zenji.
16. Ukitaka kugombana naye, mwambie kuwa hiyo simu haiselfishi - Antar, Makumbusho Kijitonyama DSM.
17. Hapa sasa mademu wote wa 'bush stars' wangu - Nahoja Mazengo, Mbande Chamazi DSM.
18. Wewe! Hebu acha ushamba wako bwana, unawaabisha Wairinga wenzip - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
19. Hiyo selfii yako inanitia homa kwa kicheko - Bimkubwa Ausi Juma, Michenzani Unguja.
20. Hilo ndio tatizo la Wahehe wakishaingia mjini - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
21. Kaa hivyo hivyo, baada ya 'masaa' kadhaa utaona sehemu ya kupigia picha inajionyesha - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
22. Watu wa kizazi hiki, kweli wamedata. Haya bhana na selfii yako bandia - Mama Nah, Manzese DSM.
23. Kweli ushamba zigo la miba. Tangulini simu hiyo ikatumika kwa selifii? - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
24. Hiyo ni sawa na kuosha mchele kwenye mto wa maji mengi. Utapata taabu sana - Semeni Mpanjira, Kilwa.

**SMS Bomba ya Leo:**
Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.

## PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0773 477 311**




## Ubaya unapolipwa duniani

**Na Adam Fungamwango**

SIKU zote mtu anapomfanyia mwenzake ubaya, basi akumbuke kuwa ipo siku naye atalipwa kwa ubaya ule ule.

Hata kama si yule aliyemfanyia, lakini siku zote mabaya hulipwa hapa duniani, bila kujali kuwa nani anamlipa.

Unaweza kumfanyia mtu ubaya Mbeya. Nawe ukalipwa na mwingine mkoani Kagera.

Hili linafanana mno na filamu hii ya 'Mchana Kweupe'. Imechezwa na Adili Addy, Sultan Mkubwa, Elias Mkali, Mussa Kinyasi, Babu Piro, Sudi Rashid na wengineo.

Esha yuko na mumewe Sultan nje anamuwekea maji ya kuoga. Wakati mumewe anaingia bafuni na yeye akaingia ndani. Cha ajabu anamkuta pia ndani. Anashangaa, anamuuliza, lakini mumewe naye anaonekana hajui nini kimetokea.

Rafiki wa mumewe aitwaye Fred anakuja kulipa deni. Mzigo unawekwa kwenye kiti. Mume wa Esha na mkewe wanamsindikiza mgeni, lakini wanaporejea hawauoni.

Ugomvi unaanza kila mmoja kumtuhumu mwenzake kuwa kauchukua. Mauzauza yanazidi kutokea ndani. Esha anapika chakula, lakini anapokuja kufunua hakikuti chakula. Hali hiyo inaanza kumchosha mume. Anamwambia rafiki yake anamtafutie mwanamke kwa sababu Esha ni mwanamke ambaye hamuelewi.


Fred anamtafutia rafiki yake Sultan mwanamke mmoja anayeitwa Vanessa. Kila kitu kinafanywa kama kilivyopangwa. Esha anapewa talaka na kuletwa mke mwingine Vanessa. Kama walidhani wametibu tatizo, wamekosea. Siku moja Fred huyo huyo anakuja kwa rafiki yake akiwa na mke mpya waliyemtafutia mwenyewe akaomba maji. Lakini maji yake yalikuwa na pilipili. Vanessa anashangaa kwa sababu kwenye maji hajaweka pilipili. Unatokea mzozo mkubwa na Fred anaondoka kwa hasira.

Suala hilo lilipopoa, Vanessa alikwenda nyumbani kwa Fred kumuomba msamaha, ikizingatiwa kuwa yeye ndiye aliyemuweka kwenye nyumba hiyo.

Wakati majadiliano yanaendelea, tukio la ajabu linatokea. Vanessa anapatwa na tatizo la kuvimba tumbo ghafla.

Fred anampigia simu rafiki yake Sultan afike nyumbani kwake. Anapofika hapo haelewi kitu, anaanzisha mzozo na rafiki yake na kumuuliza amemfanya nini mkewe, kwani si hali ya kawaida. Wakati wakiwa kwenye ugomvi, ghafla Vanessa anatoweka kimiujiza. Wote wanaacha kugombana, wanashtuka. Baadaye Vanessa anatokea kimiujiza, lakini safari hii akiwa hana tena lile tumbo.

Wote wanaanza kujiuliza, hali hii ya mauzauza inatokea kwa sababu gani? Ndipo Sultan anaporudisha kumbukumbu nyuma. Anamchukua rafiki yake Fred na kuanza kumsimulia. Miaka mingi huko nyuma alikuwa na mke kabla ya Esha. Lakini alimuua baada ya kukorofishana. Kaka wa mkewe anafika na kukuta hali hiyo, naye anauawa kuficha ushahidi. Rafiki yake anafika na kumsaidia kwenda kuzika mke na shemeji. Wakaficha siri. Lakini wote wawili Sultan na mwenzake wanaanza kupata matatizo ya mauzauza. Wanaamua kwenda kwa mganga ambaye baada ya kwenda naye hadi walipowazika marehemu aliwahakikishia kuwa tatizo la mauzauza halitowarejea tena. Hata hivyo mambo bado yanaendelea. Hivyo sasa akaamua kwenda kwa mganga mwingine ambaye alichomsaidia ni kuumaliza mzimu wa mke wa kwanza na shemeji yake ulio hali unawasumbua.



# IMETIMIA

## KYLIE, SCOTT WATUPIANA VIRAGO

HATIMAYE imetimia kwa moja ya 'kapo' maarufu kuingia katika orodha ya kusambaratika ndani ya mwaka 2019.

Kapo hiyo ni ile ya mwanamitindo Kylie Jenner na mwanamuziki Travis Scott, ambao imeelezwa wamejisalimisha kwa kila mmoja kuchukua njia yake.

Kylie Jenner na Travis Scott wanahitimisha mapenzi yao baada ya kuwapo kwa mitikisiko kadhaa katika uhai wa mapenzi yao.

Kulingana na mtandao wa TMZ wawili hao wameamua kuvunja uhusiano wao kuanzia sasa kutokana na kutokuwa karibu kwa muda mrefu.

Chanzo kinasema kwamba wapenzi hao walikuwa tofauti tangu mwezi Agosti wakati walipokuwa Santa Monica kuandaa makala yao.

Kylie na Travis yawezekana watawekа wazi suala hilo miezi michache ijayo baada ya kila mmoja kukubaliana masuala kadhaa ikiwamo matunzo ya mtoto.

TMZ pia imeeleza kwamba kulikuwa na harakati za kuokoa penzi lao, lakini wiki chache zilizopita mambo yalionekana kuharibika na kila mmoja kuamua kukaa kando na mwenzie.

Penzi lao lilikuwa na misukosuko mingi, huko nyuma walitengana baada ya kuvunja taarifa kwamba Scott ana uhusiano na mwanamke mwingine jambo lililofanya Kylie Jenner kuvunjika moyo.

Hata hivyo, Scott alikana jambo hilo kwa kueleza hawezi kumsaliti mpenzi wake ambaye ni mama wa binti yake.

# Adele azushiwa jambo zito



KWELI mitandao huzua mambo! Hayo yamemkuta mwanamuziki Adele na Skepta kuvumishwa wana uhusiano wa kimapenzi kutokana na twitter tu.

Adele ambaye ni mshindi wa tuzo ya Grammy, aliyepata umaarufu duniani kutokana na umahiri wake wa kuimba nyimbo za mapenzi, anahusishwa kutoka na rapa Skepta wote raia wa Uingereza.

Kwa mujibu wa taarifa za karibu na msanii huyo siku si nyingi Adele ataomba talaka kutoka kwa mume wake Simon Konecki . Tangu kuanza kwa uvumi huo wa Twitter mashabiki wake hawalali kwa kutoa maoni tofauti.



## Bieber kweli umemuoa mara mbili?

MENGI yamezungumzwa kuhusu ndoa ya mwanamuziki wa Pop, Justin Bieber na mke wake Hailey Baldwin. Lakini sasa kuna habari mpya nayo ni kufunga ndoa kwa mara ya pili.

Imeelezwa wanandoa hao walifunga pingu ya maisha Septemba 30 mwaka huu huko South Carolina na kufuatia sherehe ya kufa mtu ambayo ilihudhuriwa na waalikwa 154.

Baadhi ya watu maarufu waliokuwapo katika sherehe hiyo, walituma picha kadhaa ikiwaonesha wakifurahia chakula na burudani.

## Genevieve mambo yanazidi kunoga

MWIGIZAJI mkongwe wa Nigeria, Genevieve Nnaji, ataiwakilisha nchi hiyo katika tuzo maarufu ya Oscar kwa mwaka 2020.

Kupitia filamu ya 'Lionheart' ambayo yeye ameiongoza itakayoshindanishwa katika kipengele cha filamu bora ya makala.

Kulingana na orodha iliyochaguliwa Octoba 2, filamu hiyo inaongoza kwa kupendwa na watu wengi.





## Funke hayo ndio mahaba niue

ENDAPO mwanamke atakuwa na furaha kwenye ndoa yake, kila kitu katika maisha kitakwenda vizuri.

Ndivyo msanii Funke Akindele, anavyofurahia ndoa yake hadi kufikia hatua ya kuwaeleza mashabiki wake kuwa mume wake ndiyo kila kitu na hakuna mwanaume kama yeye.

Akitumia mtandao wa Instagram,Funke ambaye ni mwigizaji wa Nollywood amesema licha ya kupata watoto wawili bado anamuona mume wake Abdul Rasheed Bello kama kijana wa sasa.

## Blackface maneno yako yanachoma

MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria, Blackface ametoa ushauri kwa wasanii chipukizi kuacha kuiga muziki wa watu maarufu.

Akitoa maoni yake amesema kupitia mtandao wa kijamii kwamba wasanii hao kuacha kupiga muziki wa Fela Anikulapo Kuti kwani utawadumaza.

Lackface ilibidi kutoa ushauri huo baada ya mashabiki wake kuibua majadala kuhusu wasanii wanaoiga nyimbo za wengine.



**SAFU**



Na John Juma
0716217615

**MIONZI YA SHERIA**

# Raia anaweza kuhoji, kukataa kukamatwa

SIKU zote wananchi wamekuwa wakililalamikia jeshi la polisi kwa namna linavyoendesha shughuli zake hasa wakati wa ukamataji wa raia.

Matumizi ya nguvu, ubabe na kutofuata sheria na taratibu maalum limekuwa ndiyo tatizo kubwa kwa wananchi dhidi ya askari.

Sio siri askari wamekuwa wakitumia nguvu na ubabe mno katika kuwakamata raia.

Hata pale pasipo na haja yoyote ya kutumia nguvu bado wao wamekuwa wakilazimisha nguvu nyingi hali ambayo hupelekea vurugu , kuumizana na hata mauaji.

Mara nyingi unapochunguza matukio mbalimbali ya vurugu ambayo huwahusisha raia na polisi utagundua kwa haraka kuwa ubabe wa askari ndio uliopelekea vurugu.

Basi leo nitaeleza nini ufanye askari anapokiuka taratibu hasa wakati wa kukamata au kukuweka chini ya ulinzi.

**KUKAMATWA NI NINI?**

Sura ya 20 Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002 ndiyo sheria inayotoa mwongozo wa namna na jinsi ya kumkamata mtu.

Pamoja na hayo sheria hii haikueleza moja kwa moja nini maana ya kukamata. Hata hivyo kutokana na miongozo mbalimbali ya kimahakama ambayo hutumika kutafsiri, sheria hii tunaweza kupata tafsiri ya neno kukamatwa kwa kusema kuwa ni tendo la kumzuia kwa muda raia ambaye inatuhumiwa kwa kosa fulani, ambalo hufanywa na mamlaka husika. Kwa tafsiri hiyo tendo la kuzuia lazima liwe la muda, raia anayekamatwa lazima awe ametuhumiwa, na pia ukamataji lazima ufanywe na mamlaka. Huo ndio utakuwa ukamataji..

**MWENYE MAMLAKA**

Kwanza kifungu cha 14 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinampa mamlaka askari polisi kumkamata au kumweka chini ya ulinzi raia mtuhumiwa . Hii ni kusema kuwa mamlaka ya kukamata aliyonayo askari yeyote ameyapata kutoka kifungu hiki.

Pili kifungu cha 18 cha sheria hiyohiyo kinampa hakimu yeyote mamlaka ya kumkamata raia mtuhumiwa.

Mahakimu wamegawanyika, wapo mahakimu wa mahakama za mwanzo, mahakimu mahakama za wilaya na mahakimu mahakama za hakimu mkazi.

Hawa wote ni mahakimu na wanayo mamlaka ya kumkamata mtuhumiwa kwa mujibu wa kifungu hiki.

Tatu kifungu cha 16 cha sheria hiyohiyo kinatoa mamlaka kwa raia yeyote kumkamata mtu anayetenda kosa.

Hapa tofauti ni kuwa mamlaka ya raia kumkamata raia mwenzake ni madogo na huwezekana pale tu ambapo mtuhumiwa ametenda kosa kubwa na pengine kuna wasiwasi kuwa anaweza kutoroka asipozuiliwa haraka na kwa muda huo.

Lakini, kama mazingira si haya basi raia anatakiwa kutoa taarifa polisi ili wao wenyewe ndiyo wafanye kazi hiyo.

**MATUMIZI YA NGUVU**

Kifungu cha 21 cha sheria hiyo kinakataza kabisa matumizi ya nguvu wakati wa kumkamata raia.

Matumizi ya nguvu ni pamoja na kumpiga mtuhumiwa , kumfunga pingu, kumshika suruali kwa kumning'iza, kumtukana au matumizi yoyote ya lugha chafu na kila kitu kinachofanana na hayo.

**KUKATAA KUKAMATWA**


Sheria inaruhusu raia kukataa kukamatwa askari anapokiuka taratibu.

Katika kesi ya Nzige Juma dhidi ya Jamhuri ya mwaka 1964, mahakama ilisema kuwa ikiwa mtu atakamatwa bila kufuata utaratibu basi mtu huyo anaruhusiwa kugomea ukamataji huo.

Huu ndio uamuzi wa mahakama na kwa mujibu wa sheria uamuzi wa mahakama ni sheria na hivyo maamuzi hayo ni sheria. Kwa sheria hii nitoe mwito kwa raia kutowaonea aibu askari polisi wanaokiuka taratibu ikiwa ni pamoja na matumizi ya nguvu katika ukamataji kwa kuwagomea. Ieleweke kuwa kugoma katika hili si kuvunja sheria bali ni kutekeleza sheria. Ni haki yako kama zilivyo haki zako nyingine.

Na kugoma katika hili hakuwezi kukuletea shida yoyote na hivyo huna haja ya kuwa muoga. Kumbuka kama wewe mwenyewe hautaweza kulinda haki zako hakuna atakayelinda haki hizo kwa niaba yako. Wewe ndio unatakiwa kuwa wa kwanza kulinda na kusimamia haki zako kwa msimamo usioyumba tena bila woga huku ukiamini kuwa uko salama mbele ya sheria.

Chukua hatua sasa kwa kukataa na kugomea ukamataji uliokiuka taratibu na maelekezo ya kisheria.



Na Reubeni Lumbagala

**KALAMU YA MWALIMU**

# Familia zina deni kuwatunza wazee

KALAMU ya Mwalimu inaungana na wapenda wazee duniani katika maadhimisho ya siku ya kuwapenda na kuwahudumia wazee wetu.

Kila Oktoba 1, duniani huadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wazee. Kauli mbiu ya mwaka huu ni "Safari ya kuzeeka kwa usawa".

Kwa Tanzania maadhimisho yalifanyika katika Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara ambapo Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alikuwa mgeni rasmi.

Katika maadhimisho hayo, Waziri Majaliwa anaonyesha namna serikali ilivyojizatiti katika kuweka mazingira bora ili kuleta ustawi wa maisha ya wazee wa Tanzania.

Miongoni mwa masuala ambayo serikali inayafanya katika kuleta ustawi bora wa maisha ya wazee ni pamoja na kuwapatia vitambulisho kwa ajili ya kupata matibabu bila malipo katika vituo mbalimbali vya afya na hospitali. Hii ni kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Afya ya mwaka 2007.

Kutokana na wazee wengi kutokuwa na uwezo wa kumudu gharama za matibabu, serikali ilianzisha utaratibu wa kuwapatia wazee wa zaidi ya miaka 60 vitambulisho hasa wale wasio na uwezo wa kugharamia matibabu ili wavitumie watakapohitaji huduma za afya bila kulipa.

Utaratibu huu umewasaidia wazee kuimarisha afya zao kwa kupata matibabu stahiki na kwa wakati kwani wanapofika katika vituo vya afya hupewa kipaumbele cha kuhudumiwa bila kupanga foleni. Changamoto ya utaratibu huu ni kwamba katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu, wazee bado hawajapata vitambulisho hivi hali inayochangia kushindwa kunufaika na huduma bora za afya.

Waziri Mkuu Majaliwa pia anazungumzia namna Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) unavyonufaisha kaya maskini zikiwamo wanazoishi wazee.

Mfuko wa Tasaf unatoa ruzuku kwa kaya maskini kila baada ya miezi mitatu ili kaya hizo ziweze kuibua miradi ya maendeleo hatimaye waweze kujikomboa na adui umaskini. Waziri Majaliwa anasema "Hadi kufikia Septemba 2019, jumla ya wazee 680,056 kutoka kaya 1,118,747 wananufaika na mpango wa Tasaf kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

Mpango huu, umesaidia wazee kujikimu na kumudu majukumu ya kulea wajukuu ambao wazazi wao wamepoteza maisha kwa sababu mbalimbali yakiwamo maradhi. Pia, anasema serikali inatoa ulinzi kwa wazee dhidi ya mauaji ya vikongwe yanayotokana na imani za kishirikina.

Hii ni mifano michache tu ya namna serikali yetu inavyowalinda na kuwahudumia wazee ili kuwafanya wafurahie maisha na waone duniani ni mahali salama kwao kuendelea kuishi.

Pamoja na kazi kubwa na nzuri iliyofanywa na inayoendelea kufanyika na serikali yetu katika kuwahudumia wazee, ni lazima familia na jamii zitimize wajibu wao kikamilifu katika kuwahudumia wazee ili kuipunguzia serikali mzigo wa kuwahudumia wazee.

Si jambo la afya kuona wazee wanaishi katika kambi maalum za kuwalea ilihali wanafamilia wa mzee huyo wako hai na wana uwezo wa kumtunza baba au mama yao. Ni ukweli usio na shaka kuwa wazee wametoka katika familia, hivyo wanafamilia watimize wajibu wao wa kulea wazee kwani wazee hao kipindi cha ujana wao walishiriki katika kuwatunza wanafamilia ambao kwa sasa wanalikimbia jukumu hilo na kuiachia serikali pekee.

Tukiwa katika mwendelezo wa kuadhimisha Siku ya Wazee Duniani; familia na jamii ijiulize namna watu wanavyotimiza wajibu wao wa kuwalea wazee wao. Ikumbukwe kila mzee alikuwa kijana na kila kijana ni mzee mtarajiwa. Hivyo basi, kila mwanafamilia na mwanajamii ione deni kubwa alilonalo katika kuwatunza wazee walio nje ya familia na jamii yake. Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 inaonyesha kuwa familia na jamii zina wajibu wa msingi wa kuwatunza na kuwalea wazee.

Ni jambo la kuzingatiwa kuwa suala la kuwalea na kuwatunza wazee linaanzia katika ngazi ya familia na jamii kabla ya kufikia ngazi ya kuhudumiwa na serikali.

Aidha, mtu binafsi au mashirika yasiyo ya kiserikali yanaweza kushiriki moja kwa moja katika kuwasaidia wazee kama kundi maalum katika kuwapatia wazee mahitaji ya msingi kama vile, chakula, mavazi, malazi, matibabu nk ili nao wafurahie maisha.

Wazee wametumia muda mwingi katika maisha yao kulitumikia taifa na kuchangia moja kwa moja katika maendeleo yake kuanzia pengine kabla na baada ya uhuru.

Kuwasahau na kushindwa kuwatunza wazee ni kushindwa kuthamini mchango wa wazee hawa katika taifa lao. Njia bora na ya pekee ya kuthamini kazi na mchango wa wazee katika taifa letu ni kuwatunza na kuwapatia mahitaji muhimu katika muda uliobaki wa maisha yao.

Tukifanya hivi, tutawafurahisha wazee wetu na Mungu pia na hatimaye Mungu atatubariki. Tafakari.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.

**Kwa maoni na ushauri: (+255) 764 666349.**

## MOTO WA ELIMU

# Wazazi hulipa walimu posho kila mwezi, mbunge achangia 50,000/-

**Na Sabato Kasika**

KILA mzazi au mlezi ana ndoto ya kumfikisha mwanaye kwenye kilele cha taaluma anayoitamani, akilenga kumsomesha kwenye mchepuo anaoutaka. Uwe wa sanaa au sayansi.

Masomo ya sayansi yamekuwa na changamoto nyingi kuanzia vifaa, maabara, vitabu na kubwa zaidi uhaba wa walimu, shida inayozitesa shule nyingi za umma.

Kama wanafunzi wa shule za serikali ndiyo wanaokabiliwa na uhaba huo, wazazi na walezi watatimizaje azma ya kuwapaisha watoto kileleni ili kufikia taaluma wanayoitaka?

Wazazi na walezi wa baadhi ya wanafunzi wameamua kuchangishana fedha kwa ajili ya kuwalipa posho walimu wa kujitolea kufundisha sayansi.

Hili, limetokea katika Halmashauri ya Wilaya Musoma mkoani Mara, ambako mzazi au mlezi mwenye mtoto anayesoma sayansi huchanga kati ya Sh. 400 na 1,000.

Japo ni kwa baadhi ya shule, wazazi na walezi hao wanakabiliana na ukosefu wa walimu wa fizikia, hisabati, bailojia na kemia kwa kutoa michango kila mwezi ili kuwalipia walimu wa kujitolea wanaofundisha masomo hayo.

"Wazazi na walezi hawa wamekubaliana kuwalipa posho wanaojitolea.Wanalenga kuinua kiwango cha elimu katika sekondari zilizomo katika Halmashauri ya Wilaya ya Musoma na kuongeza ari ya kusoma sayansi," ni kwa mujibu wa Charles Magoma, mwenyekiti wa halmashari hiyo.

Anasema motisha hiyo inawafikia walimu wa sekondari nne za kata na kwamba jitihada zinafanywa ili kuzihusisha sekondari zote 18 za halmashauri hiyo.

Anataja zinazonufaika kuwa ni pamoja na Bukima, Nyanja, Kiriba na Nyakatende kati ya shule 18 na kwamba wanaojitolea ni walimu waliomaliza masomo lakini hawajapata ajira.

**KIWANGO CHA UHABA**

Magoma anasema wanafunzi wa sekondari ya Bukima kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne wana walimu watatu wa fizikia lakini mmoja ni wakujitolea.

Aidha, kemia wapo walimu watatu wawili ni wa kujitolea, hisabati ni wawili na mmoja anajitolea wakati baiolojia wapo walimu wawili na mmoja akiwa anajitolea.

Nyanja sekondari yenye kidato cha kwanza hadi cha nne, walimu wa fizikia ni wawili japo mmoja anajitolea.

Kadhalika, kemia na hisabati kuna walimu wanne lakini wawili ni wa kujitolea wakati baiolojia ina mwalimu mmoja na wanahitajika wa kujitolea.

Magoma anasema karibu sekondari zote 18 kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne walimu ni wachache ni aidha, wawili au mmoja na kwingineko hawako kabisa.

**MCHANGO WA POSHO**

Mwenyekiti huyo anasema katika Sekondari ya Bukima kila mzazi na mlezi mwenye mtoto anayesoma sayansi anatoa Sh. 1,000 kila mwezi kwa ajili ya posho ya walimu wanaojitolea.

Anasema Nyanja wamekubaliana kila mmoja kutoa Sh. 900 kwa mwezi, wakati wenzao wa sekondari ya Kiriba wanachangia Sh. 1,000 kila mmoja kwa mwezi na Nyakatende wamejiwekea kila mmoja dau la Sh. 400 kwa mwezi .



Naibu Waziri wa Elimu, William Ole Nasha (wa pili kulia) akiwa kwenye ukaguzi wa shule ya Sekondari Kasoma, Musoma Vijijini. Wengine ni Kaimu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, Ibrahimondi Malima (wa kwanza kulia) na Mkuu wa Wilaya ya Musoma Dk. Vincent Anney (wa pili kushoto).

**MCHANGO WA MBUNGE**

Wakati wazazi wakichangia kiasi hicho kila mwezi, Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo, anatoa Sh. 50,000 kwa mwezi kwa kila shule, kiasi alichotoa kuanzia mwaka huu wa 2019 na kwamba anazisadia shule nne ikiwamo Bugwema ambayo wazazi na walezi hawawachangii walimu hao.

"Kwanza ieleweke kuwa shule hizi ni zetu wazazi, hivyo wakati serikali ikiendelea na mchakato wa kuajiri walimu zaidi, sisi tumeona tuwe na utaratibu huu wa kuchangia posho kwa walimu wa kujitolea," Prof.Muhongo anasema.

Anaeleza kuwa utaratibu wa kulipa posho umeanza katika shule hizo chache na anaamini utakuwa chachu kwa wazazi wengine na hatimaye shule zote 18 zitakuwa na walimu wa aina hiyo hapo baadaye.

"Jambo la msingi ni uhamasishaji tu na bado tunaendelea nao kwa wazazi wa kata nyingine, kwani Musoma Vijijini ina kata 21 na sekondari 18, penye nia pana njia," anasema.

**MAONI YA WAZAZI**

Anna Elias ni miongoni mwa wazazi waliojitolea kulipa Sh. 1,000 kila mwezi kuwapo motisha walimu wa Bukima, anaeleza kuwa kila mdau ana sehemu kuchangia na hivyo haoni tatizo kuchangia Sh. 1,000 kila mwezi kwa ajili ya maendeleo ya watoto wao.

Magesa Ebajiro wa Kijiji cha Nyakatende, anasema wamekubalina kuchangia Sh. 400 kila mmoja kwa mwezi japo ni kidogo lakini ni kutokana na uhaba wa mapato lakini kiasi hicho kitaongezeka.

Ebajiro anasema, Kata ya Nyakatende ina vijiji vinne, hivyo watu wakitoa kwa uaminifu kila mwezi, walimu wa kujitolea watapata chochote cha kuwasaidia wakisubiri ajira.

**MIKAKATI YAKUBALIKA**

Majidu Kalugendo, ni Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Musoma, anasema mikakati hiyo ni miongoni mwa jitihada za wazazi na walezo waliyoweka kuboresha elimu kwenye sekondari zao.

"Hizi shule ni mali ya wazazi, wameamua kujipanga kimkakati, ambao lengo lake ni kuboresha masomo kwa kuongeza walimu wa kujitolea, hili ni jambo jema," anasema Kalugendo.

Anasema, wazazi wana mikakati mingi kwenye eneo la elimu, ikiwamo kuongeza kidato cha sita kwenye baadhi ya sekondari za kata, na kwamba mchakato unaendelea kwa ajili ya kufanikisha hilo.

Miongoni mwa yale yanayoendelea ni kuboresha miundombinu muhimu ya shule kabla ya kuwa na kidato cha tano hadi cha sita, kwa hiyo wadau wa elimu wanakaribishwa kuwaunga mkono," anasema.

**UHABA WA WALIMU**

Kwa mujibu wa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, taifa lina uhaba wa walimu 80,000, huku 14,000 wakiwa ni wa sekondari na 66,000 wa shule za msingi.

Akijibu swali bungeni jijini Dodoma Mei mwaka huu, Naibu Waziri huyo anasema changamoto inatokana na sababu mbalimbali ikiwamo walimu hewa, uhamisho na kufariki dunia.

Kwa kutambua matatizo hayo, ajira zilizofanywa baada ya serikali kujiridhisha zilikuwa ni za kuziba nafasi na kwamba zinazofuata zitakuwa ni za kupunguza pengo la mahitaji halisi, anasema Naibu Waziri Waitara.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Bukima wakiendelea na masomo darasani.



Walimu wa Sekondari ya Rusoli wakiwa na vifaa vya maabara walivyopokea kutoka kwa mdau wa maendeleo ya elimu.

**PICHA ZOTE: MTANDAO**

MAKALA

# TIGO SAIZI YAKO

# Wateja sasa milion 11+, ni ubia kuzalisha simujanja, bei nafuu

Na Mwandishi Wetu

MAENDELEO ya sayansi na teknolojia duniani yamesababisha mahitaji ya huduma za mitandao hasa intaneti kuongezeka kila wakati.

Kupitia mawasiliano ya simu na intaneti wengi wamenufaika wakulima na wafanyabiashara kupata na kufikia masoko, wanafunzi kujisomea mitandaoni na karibu kila kundi kwenye jamii lina cha kujivunia.

Ni kutokana na ukweli kuwa intaneti imekuwa kiungo muhimu cha mawasiliano baina ya watu, taasisi na mashirika huku ikiwezesha upatikanaji wa taarifa kuwa wa rahisi na haraka zaidi kuliko kipindi kingine chochote.

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ueneaji wa intaneti nchini umeongezeka kutoka asilimia 40 mwaka 2017 hadi kufikia asilimia 43 mwaka 2018.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa ongezeko hilo linachangizwa na kuwapo na idadi kubwa ya watumiaji wa simu za mkononi wanaopata huduma kutoka kwa watoa kampuni za simu jambo linalorahisisha upatikanaji wa intaneti kwa watu wengi zaidi kwa wakati wote.

Kati ya watoa huduma hao nchini ni kampuni ya Tigo ambayo kwa sasa inashika nafasi ya pili kwa ukubwa ikiwa na wateja wengi zaidi.

**MWANZO KIMAFANIKIO**

Kwa mujibu wa takwimu za TCRA Tigo ina wateja takribani milioni 11.6.

Ofisa Biashara Mkuu wa Tigo, Tarik Boudiaf, anasema safari ya Tigo katika kuleta suluhu kidigitali kwa wateja wake ilianza baada ya kampuni hiyo kufanya mageuzi ya kiuendeshaji na kuifanya kuwa kampuni ya kidigitali ikitoa bidhaa mbalimbali pamoja na intaneti ya kasi mbali na kuhudumia wateja kwenye kupiga simu, kutuma meseji na huduma za kifedha mitandaoni.

Anasema kuwa kampuni hiyo ni moja ya waanzilishi wa teknolojia ya intaneti yenye viwango vya kimataifa kupitia mtandao wa 2G na 3G.

"Tigo imekuwa ya kwanza kuanzisha intaneti yenye kasi ya 4G-LTE na kuiboresha kwenda 4G+, jambo ambalo limedhihirisha utayari wake katika kuleta mapinduzi ya kidigitali hapa nchini,"anasema.

Anaeleza kuwa kupitia dhamira yake ya kuleta mapinduzi ya kidigitali Tigo inakuwa mmoja wa kampuni za juu zenye kuchochea ueneaji na matumizi ya intaneti kwa wateja wake.

Anafafanua kuwa kupitia mkakati maalumu, Tigo imeanzisha jitihada mbalimbali ambazo zimebadilisha mwenendo wa soko huku ikichangia katika agenda ya ujumuishwaji wa watu kidigitali nchini.

"Mkakati wetu ni kuendelea kuleta ujumuishwaji wa kidigitali na kuboresha mfumo wa maisha Tanzania.Tigo ni kampuni ya kwanza kuanzisha intaneti ya 4G na hivi karibuni imeleta teknolojia ya 4G+ iliyozinduliwa chini ya kampeni ya "always a step ahead".

" Hii inadhihirisha nia yetu ya dhati ya kuwaunganisha Watanzania na intaneti ya kasi na ya uhakika huku tukiwajengea uelewa juu ya faida za huduma hii ya mtandao," anasema Boudiaf na kuongeza:

"Tunatambua kwamba wateja wetu wanahitaji huduma ya uhakika na yenye ufanisi ambayo inahusisha teknolojia yenye miundombinu ya hali ya juu, vifurushi mahsusi pamoja na simu janja (smartphones) za kisasa pamoja na kuwapa maudhui yenye uhalisia."

Anaongeza kuwa kampuni hiyo imewekeza sana kwenye ujenzi wa miundombinu ya teknolojia ya intaneti ya 4G ambayo imeboreshwa na kuwa 4G+ na hatimaye kukidhi mahitaji ya huduma za mtandao na kukuza teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) kwa Watanzania.

Anasema kwa mujibu wa Takwimu za Taasisi ya Kimataifa ya GSMA (inajishughulikia masuala ya simu za mikononi na kuwasilisha matakwa ya watumiaji wake kwa wadau ikiwamo serikali) za nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ya mwaka 2019, inaonyesha kuwa matumizi ya simu janja yataongezeka mara mbili ifikapo mwaka 2025.

Ukanda wa Afrika Mashariki unatajwa kushuhudia ongezeko kubwa zaidi. Ripoti inaziibua Rwanda na Tanzania kuongoza kwenye ukuaji huo.

**SIMU NAFUU**

Ofisa Biashara Mkuu, Boudiaf, anasema kutokana na ukweli kuwa matumizi ya mtandao hufanyika kupitia simu za mkononi hivyo upatikanaji wa simu za bei nafuu ni chachu katika kuchochea ueneaji wa intaneti nchini.

"Tigo imetengeneza mkakati madhubuti wa kuchochea matumizi ya simu janja kwa watu wote.Tunaamini kuwa kuingia ubia na wazalishaji wa simu za mkononi kama Samsung, Tecno, Nokia, Infinix na Itel kumechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza gharama za simu na kuzifanya zipatikane kwa urahisi hadi kwa watu wenye kipato cha chini." Anasema.

Anaongeza kuwa Tigo imekuwa ikiendesha kampeni mbalimbali zenye lengo la kutoa simu kwa wateja ikiwamo ile ya 'Wagiftishe' na hivi karibuni imekuja na kampeni ya 'Lamba Dume' ambazo mbali na kutoa simu, zinawapa wateja fursa ya kupata intaneti ya bure inayodumu kwa takribani mwaka mmoja.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, ijapokuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye tozo ndogo za intaneti kwenye ukanda huo, suala la kutengeneza vifurushi nafuu vya intaneti ni jambo la msingi. Mfano; kifurushi cha 'Saizi Yako' ni moja ya 'bando' ambalo linavyolenga kumpa mteja huduma ya intaneti bila mipaka na anaweza kujipatia intaneti kulingana na mahitaji yake.

Anasema upatikanaji wa maudhui ya ndani ni moja ya sababu za kuongeza matumizi ya intaneti.



Ofisa Biashara Mkuu wa Tigo, Tarik Boudiaf

Tigo inatoa vifurushi mbalimbali ambavyo vinaruhusu wateja kujipatia maudhui yenye kukidhi mahitaji ambapo kupitia mtandao wa You Tube, StarTimes na DSTV wateja wanaweza kuunganishwa na chaneli hizo na kufurahia maudhui yenye uhalisia wa ndani.

HUDUMA KURIDHISHA

Kuhusu suala la uridhishwaji wa huduma za mtandao zinazotolewa na kampuni hiyo, Boudiaf anasema "Kupitia kufanya uvumbuzi mbalimbali, Tigo inalenga kuhakikisha wateja wetu wanapata huduma bora na zenye viwango kupitia bidhaa na huduma za kisasa kila wanapokutana na nembo yetu.

"Uwekezaji wa Tigo kwenye intaneti ya 4G umehakikisha upatikana kwa intaneti ya uhakika na yenye viwango stahiki, nia ni kuiweka sekta ya mawasiliano kwenye viwango vya juu na kuleta mageuzi ya kidigitali," anasema.

Anaeleza kuwa Tigo Tanzania inajinasibu kwa kuongoza soko katika kuchochea maendeleo ya digitali na zaidi katika kuleta huduma zenye kukidhi mahitaji ya wateja na hii imesababisha kutengeneza huduma na bidhaa zenye kukidhi mahitaji ya soko la Tanzania.

Anasisitiza kuwa wateja wa Tigo wanafikiwa kote nchini kupitia njia mbalimbali ikiwamo maduka ya Tigo, dawati la huduma kwa wateja pamoja na mitandao ya kijamii ikiwamo facebook, twitter, whatsApp na Instagram ambayo inampa fursa mteja kushiriki katika uboreshaji wa huduma kwa kutoa maoni juu ya huduma zitolewazo na kampuni hiyo.

Anasema fursa ya kuwaunganisha Watanzania na huduma ya intaneti ya uhakika bado inatakiwa kupewa kipaumbele kutokana na ukweli kuwa bado idadi kubwa ya watu wanakaa nje ya mtandao au offline na hilo Tigo wanalifanyia kazi kwa bidii.

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 14 00)



Dondoo: Kulia
1. Nchi kubwa barani Afrika
5. Kinyume cha ubaya
6. Nchi isiyo mwanachama wa Umoja wa Afrika
8. Husababishwa na mafua
9. Pesa ya kuendesha miradi
13.Heshima 14.Msitu mkubwa duniani 15.Jambo unaloahidi kufanya 16.Ugwe 18.Mwamuzi wa kesi 21.Mwandani
23. Dhamira 24.Neno la kukataa jambo 27.Shilingi ya kihindi 29.Nyenyere 30.Wingi wa mguu 31.Funga nikaha
32.Tunda dogo lifananalo na fuu

Dondoo: Chini
1. Mji mkuu wa Eritrea
2. Jela 3.Poswa 4.Sehemu ya kitu
7. Msiba 8. Pania
10.tendo la kumchukulia mtu dhamana 11. Utemi
12.Kiongozi dini ya Kiyahudi
14.Pigwa 17. Mkakati
19.Shauri liendalo mahakamani
20.Kimiminika 22.Fuata amri
23.Kifupi cha na mimi
25.Tamka maneno kimuziki
26.Badilishwa kwa fedha
28. Kagua

Jibu Na: 13



# Jamii ilivyosalimu amri ikakoma ukeketaji Dar

Na Salome Kitomari

WATU huhama na tabia, tamaduni na mila zao ambazo wanaamini ni lazima zitekelezwe popote wanapokuwa, bila kujali zipo ambazo zina madhara na zinakatazwa kisheria kwa kuwa pia zinakiuka haki za binadamu.

Wakati mwingine ni vigumu kuamini kwamba ukeketaji unaweza kufanywa mijini, kwa kuwa imezoeleka maeneo yanayoendeleza mila hiyo ni yale ambayo hajayapata uelewa wa kutosha wa kuziwezesha fahamu zao kujua kuwa hata wanawake wasipokeketwa ili kuitii mila hiyo hakuna madhara yanayoweza kutokea.

Kwenye jamii zinazokeketa watoto wa kike wanataja sababu kuu kuwa ni kumfanya binti atulie na mwanamume mmoja, kumuandaa kuwa mke wa flani ambaye ataipa familia heshima na mali nyingi kama ng'ombe kwa kuwa wapo ambao hutoa mahari ya ng'ombe 500.

Wengine huamini ni kutibu ugonjwa wa njia ya haja ndogo uliopachikwa jina la lawalawa ambao kimsingi humpata mtoto akiwa katika umri wa kutambaa, asiposafishwa vyema sehemu za siri, uchafu hutengeneza vijidudu na kumletea madhara.

Jamii hiyo huamini kuwa kwa kukata sehemu hiyo mtoto huyo atapona, kumbe suluhisho ni kumpeleka hospitalini na kupata tiba sahihi kwa wakati sahihi.

Imani nyingine ni kuongeza utajiri kwenye familia, kwamba kama familia ina watoto wa kiume watahitaji ng'ombe wengi wanapofikia kuoa, lakini kama dada zao wataolewa wakiwa wamekeketwa maana yake thamani yao imeongezeka na mali zitaongeeka zizini.

Pia, ipo imani kuwa nyama inachokatwa kwenye sehemu ya mtoto wa kike kikirushwa kwenye zizi la mifugo basi kutakuwa na uzao wa kutosha kwa familia hiyo.

Na wapo wanaoamini kwamba binti asipokeketwa ni laana kwa familia na ukoo kwa ujumla na upo uwezekano wa vifo na majanga mengine kutokea.

Yote hayo yamefanyiwa utafiti na kubainika kuwa ni mbinu za kumdidimiza mtoto wa kike kwa kuwa wapo wanaotoka kwenye familia hizo na hawajakeketwa lakini familia zimekuwa na utajiri wa mali, hakuna vifo wala laana.

Selemani Bishagazi, Mkurugenzi wa asasi ya kirai ya Sauti ya Jamii kata ya Kipunguni jijini Dar es Salaam, anathibitisha jinsi jamii ya Wakurya katika eneo hilo ilivyohama na mila za ukeketaji zinazoathiri hatma ya masomo ya mabinti wengi ambao badala ya kusoma huandaliwa kuwa mke wa mtu.




Wadau wakiandamana kupinga na kuhamasisha jamii kukataa ukeketaji. **PICHA: MTANDAO**

### URAGHIBISHI

"Mwaka 2010 nilipohamia Kipunguni nikakutana na sherehe za ukeketaji iliyofanyika kama shughuli ya ubatizo au kipaimara. Watu hutoa michango na kualikwa kwa wingi kula na kunywa," anasema.

Anaendelea: "Siku moja nilikuwa miongoni mwa wanaume walioombwa kumshika binti wa kidato cha sita aliyewashinda nguvu mangariba yaani alikuwa hataki kukeketwa, nilishiriki kumshika mguu na kuona anavyokata, wakati anafanyiwa hayo wazee wa mila wapo pembeni wanakunywa na kula," anasema Selemani Bishagazi.

Anasema ilikuwa ni siku ngumu mno katika maisha yake na picha hiyo haijawahi kumtoka kichwani na siku zote alisikia ukeketaji lakini hakujua kinachofanyika.

"Nilifikiri sana nifanye nini kuisaidia hawa wasichana, nilibaini upo uhusiano mkubwa kati ya umaskini na ukeketaji. Niliomba nafasi ya ujumbe wa nyumba 10. Niliupata ndipo nikawakusanya viongozi mbalimbali isipokuwa wanasiasa ambao wanaogopa kulizungumzia suala hilo wakihofia kukosa kura," anasema.

Anaeleza kuwa inapofanyika sherehe ya ukeketaji ni manufaa kwa wengi kuanzia wazee wa mila, ngariba, wapiga ngoma, waendesha bodaboda, wenye maduka ya bidhaa na wanaotoa huduma mbalimbali.

"Siku moja nilipita eneo la mradi wa umeme wa gesi ambalo liko wazi linaloweza kutumiwa kulima mboga, niliwaomba wamiliki kufanya kilimo walikubali, niliwakusanya wanawake na kuunda kikundi cha kilimo cha mboga.Kwa sasa mboga za Kipunguni ni maarufu baada ya kubainika madhara ya kemikali kwenye mboga za maeneo mengine," anasema Selemani Bishagazi.

Anasema mmoja wa wanawake alilima na kupata Sh. 400,000 alimshukuru kwa kupata fedha za kujivua ndoa (apewe talaka), yaani alishatengana na mumewe lakini alikuwa anadaiwa fedha za mahari zilizotolewa na maisha yake yalikuwa hatarini.

Anasema kikundi hicho kimewasaidia wanawake wengi kurejesha fedha za mahari na kuwa huru dhidi ya mateso na mabinti waliokimbia ukeketaji zaidi ya 170 wameokolewa na sasa wanaendelea na maisha yako huku wengine wanasoma.

"Kikundi chetu kinafanya shughuli nyingi za kutengeneza kipato kama kulima mbogamboga na kununua vifaa vya ufundi cherehani, vya kupika keki na upambaji kwenye sherehe, pia wamepata wataalamu wamewafundisha ujasiriamali, maadili na maisha kwa ujumla na sehemu ya faida inakwenda kwenye kikundi," anasema.

Anaeleza kuwa wasichana waliokimbia ukeketaji, waliokeketwa, wazazi na ngariba wanaanza kuwa waelimishaji ambao wanaeleza visa mkasa, ikiwamo kuweka wazi mabinti waliofariki wakati wa ukeketaji na kinachoendelea kwenye jambo hilo.

"Ukeketaji umeanzishwa na jamii yenyewe na ndiyo wanaopaswa kuumaliza," anasisitiza.

### WANAWAKE /UONGOZI

Selemani Bishagazi anasema siasa imekuwa na changamoto kwa kuwa wanasiasa wanaogopa kuzungumzia ukeketaji kwa hofu ya kukosa kura.

Anasema ndiyo maana wameona wawatumie mabinti wenyewe kulisemea kwa kuhakikisha kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa tuna viongozi wengi wanawake ambao wanapinga mila hii.

"Tunaamini mabinti hawa wakiwa viongozi watasimamia agenda hii hadi kwenye uchaguzi wa madiwani na mbunge kwamba anayeomba kura aeleze atafanya nini kuukomesha," anasema.

Kwa mujibu wa Bishagazi, utafiti waliofanya umebaini kuwa kuwa asilimia 60 hadi 70 ya jamii hiyo inapinga ukeketaji na uwepo wa wazee wa mila na kwamba awali ilikuwa ngumu kuwakabili ila kwa sasa wanaapishwa wasifanye vitendo hivyo vinginevyo watapelekwa kwenye vyombo vya dola.`

"Tunawataka wazee hawa wajivue kimila. Mwaka 2012 tulisikitika sana tulimuokoa binti, alisoma kipeperushi chetu kuhusu ukeketaji, akaikatalia familia yake na kuja kwetu kutueleza. Tukamwambia akiona dalili akimbie, lakini bahati mbaya walivyoona anakimbia mara kwa mara walimwambia hawatamfanyia tena atulie, lakini walimvizia akienda kuteka maji wakiwa wameshaandaa kila kitu alikeketwa na kupelekwa kwa mume moja kwa moja,"anabainisha.

### MAHUSIANO

Bishangazi anasema iwapo ngariba wakati wa kukeketa atakuta binti alishafanya mapenzi, familia yake hudaiwa faini ya ng'ombe wawili ambao huuzwa kwa wanunuzi wa machinjio ya Vingunguti kwa bei rahisi, na kwamba ni kama biashara yenye mnyororo mrefu.

"Wauza ng'ombe wamekuwa adui zetu, wanasema tunaharibu biashara yao kwa kuwa ilifikia mahali binti hajawahi kufanya mapenzi, ila ngariba anagoma kumkeketa kwa kudai ameshafaya kitendo hicho na kutaka faini ya ng'ombe ambao huuza kwa haraka na kupata fedha," anasema.

"Tunaamini iwapo kila mtu kwenye kata atachukia ukeketaji itafikia mahali utatoweka. Wanaotuchukia kwasababu za kiuchumi tunaendelea kuwaelimisha madhara wanayopata watoto na hatari iliyopo mbele, wanatuelewa na sasa wanaogopa kukeketa hadharani,"anasema.

Anasema baadhi ya wanajamii wa kikurya wakiona binti wanaona mali yaani ng'ombe, na kwamba matamanio yao ni kufikia wakati wa kubadili fikra zao na kuona wasomi, madaktari, mainjinia na wafanyakazi wa sekta mbalimbali ambao wanamchango kwa maendeleo ya nchi.

HABARI KIMATAIFA

# 13 wafariki ajali ya basi Kisumu

**KISUMU, Kenya**

WATU 13 wamepoteza maisha na wengine kadhaa kujeruhiwa katika ajali ya basi lililokuwa linatoka soko la Awasi Kisumu kuelekea Nairobi nchini Kenya.

Ajali hiyo ilitokea saa 5:30 usiku, juzi Alhamisi, kwa mujibu wa gazeti la Daily Nation la Kenya.

Lilimnukuu Kamanda Polisi wa Mjini Kisumu, Benson Maweu, akithibitisha kuwa kuwapo na miili ya watu waliokufa katika ajali ya basi la Eldoret Express.

"Basi lililokuwa linasafiri kutoka mji wa Kericho kuelekea Kisumu, Barabara ya Nairobi lilipata ajali lilipokuwa linalipita lori," shuhuda Maweru alinukuliwa na Daily Nation.

Kamanda wa polisi alisema kuwa kati ya watu hao 13 kulikuwa na mtoto mmoja na kwamba abiria 12 walikufa papo hapo kwenye basi na kwamba dereva wa lori naye alipoteza maisha. Ripoti ya polisi nchini humo ilisema kuwa basi hilo lilikuwa na abiria 51, na ajali imesababisha abiria 11 na madereva wote wawili wa basi na lori wamefariki.

BBC



Mabaki ya gari lililoua Kenya: **PICHA: DAILY NATION**



Hunter Biden (kulia) baba yake Joe.**PICHA: BBC**

# Maandamano uchukuzi kuzidi kutisika Mombasa

**MOMBASA, Kenya**

WAFANYABIASHARA wa kampuni za kibinafsi ya shughuli za uchukuzi bandarini Mombasa, wamepinga amri ya serikali ya agizo linalolazimisha makasha ya mizigo inayoingia bandarini Mombasa kubebewa na reli ya kisasa (SGR).

Wafanyabiashara mbali mbali wakiongozwa na mwenyekiti wa vuguvugu la jamii ya wafanyabiashara la Fast Action, Salim Karama, walisema hawakuhusishwa katika kikao cha maamuzi hayo na pia tangazo la waziri halikujali waliofutwa kazi sawa na kwamba agizo linalolazimisha mizigo kubebwa na SGR si sheria bali maamuzi ya mamlaka ya ukusanyaji ushuru na mamlaka ya bandari.

Katibu Mtendaji katika vuguvugu hilo Harriet Muganda, aliwakana viongozi wa Mombasa waliohudhuria kikao hicho kilichotoa tamko la kusimamishwa kwa muda kwa uchukuzi wa mizigo kupitia SGR, akieleza kwamba viongozi hao walioongozwa na Gavana Hassan Joho siyo wawakilishi wa wafanyabiashara na wala hawana ukweli katika kuwatetea wana Mombasa kuhusu SGR.

Walisema mipango maalum inayojumuisha kila mtu katika sekta ya uchukuzi inahitajika na si maamuzi ya mtu mmoja.

Wafanyabiashara hao wameshikilia msimamo wa kuendelea na maandamano yao Jumatatu wakati kongamano kwenye Uwanja wa Tononoka kwenye sherehe ya kitaifa ya mashujaa.

Sherehe hiyo hufanyika Oktoba 20, ambapo Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta ataongoza wananchi katika maadhimisho hayo kwenye bustani ya Mama Ngina mjini Mombasa.

Juzi Waziri wa Uchukuzi, James Macharia akiwa na viongozi wa Mombasa alisema agizo hilo liliwahi kusimamishwa miezi kadhaa na kwamba hadi sasa wanasisitiza kusimamishwa kwake.

Alisema japo wafanyabiashara hao wanasema jambo hilo halitekelezwi kwa sababu uchukuzi wa mizigo unaendelea.

Gavana wa Mombasa, aliitaka Wizara ya Uchukuzi kuweka mipango maalum inayojumuisha kila mdau katika sekta ya uchukuzi kuhakikisha uchukuzi wa mizigo kupitia reli ya kisasa unafanyika kwa njia ya kumfaa kila mfanyabiashara, kuinua uchumi wa Mombasa na wananchi wake. **DW**

# Rais Trump, Biden wazidi kukabana

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani Donald Trump, ambaye tayari anakabiliwa na shutuma inayoweza kumuondoa madarakani baada ya kumtaka Rais wa Ukraine kumchunguza mpinzani wake Joe Biden, na sasa inasemekana kuwa aliwataka China wafanye pia uchunguzi huo.

Aliziambia nchi zote mbili, China na Ukraine kumchunguza Biden ambaye ni kinara wa chama cha Democratic anayetaka kuwania urais lakini pia na mtoto wake, anatakiwa achunguzwe.

"China inapaswa kuanza kumchunguza Biden," alisema Trump.

Aidha, Democrats inamshutumu Rais Trump kwa madai ya kutoa msaada wa kijeshi kuwa njia ya kumfanya aweze kuibua mabaya ya Biden.

Biden alijibu kupitia ukurasa wake wa tweeter kuwa Trump ana wazo la kumshambulia mtu yeyote mwenye msimamo ni utani.

Mazungumzo ya simu kati ya Rais Trump na kiongozi wa Ukraini Volodymyr Zelensky, Julai 25 mwaka huu, yalipelekea wapelelezi kupeleka taarifa zinazoweza kumuondoa Trump madarakani.

Ingawa siku ya Alhamisi wiki hii , Rais Trump alidai kuwa madai hayo ni upuuzi.

Katika ujumbe wake wa usiku wa manane kupitia kurasa yake ya tweeter, Trump aliongeza kuwa yeye ana jukumu la kuchunguza kashfa za rushwa, jambo ambalo linajumuisha na kuuliza na kutoa mapendekezo kwa nchi jirani kutoa msaada.

Trump alimshutumu Biden na mtoto wake Hunter kwa kashfa za rushwa katika mikataba yao ya kibiashara na kisiasa nchini Ukraine na China , bila ya kutoa ushahidi wa kuthibitisha madai yake.

Wakati ambao Hunter Biden alipoingia katika mkataba wa gesi asilia katika kampuni ya Burisma mwaka 2014, maswali mengi yaliibuka kuwa angeweza kuleta mgogoro wa kisiasa na baba yake.

Ukraine ilikuwa inakabiliana na mgogoro wa kisiasa baada ya kiongozi wake kulazimishwa kuondoka madarakani, huku Biden akiwa katika ngazi za juu za utawala wa Obama.

Mwaka 2016, Joe Biden aliishinikiza serikali ya Ukraini kumfukuza mwendesha mashitaka Viktor Shokin, ambaye ofisi yake ilikuwa inaichunguza kwa karibu mmiliki wa kampuni ya Burisma.

Katika hotuba yake mwaka jana Biden alijisifia kwa kumfukuza Shokin na kutishia kutotoa mkopo wa mamilioni ya fedha kwa Ukraine.

**BBC.**

# HADITHI

# Jumba Jekundu-21


WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawatajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.

Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

**Na Adam Fungamwango,**

**(0716 350534)**




Alikutana na picha moja ambayo awali hakuitilia maanani, kutokana na akili yake kuelekea zaidi kusoma habari muhimu za kitaifa.

Alitaka kuhakikisha kuwa kile alichokiona ni sahihi. Aliona kama anafanisha. Chini ya picha kuna maandishi.

Aliyasoma ili kuthibitisha kile alichokiona. Hakukuwa na tofauti yake ya maelezo na picha yenyewe.

Juu ya picha kulikuwa na kichwa cha habari. Nacho pia kilisadifu kile alichokiona.

Kijasho chembamba kilimtoka. Hakuamini. Alitaka kile anachokiona kiwe ni ndoto au tamthilia na si tukio halisi.

Moyo wake aliongezeka mapigo. Wakati mwingine yalionekana kupiga katika hali isiyo ya kawaida. Yalipiga zaidi ya mara moja, juu ya muda wake wa kawaida.

Mikono ilianza kucheza, na kukosa nguvu hata ya kuendelea kulishika gazeti, likaanguka.

Akainama kivivuvivu na kuliokota tena. Alifungua tena pale pale. Akaangalia kana kwamba ndiyo anatazama kwa mara ya kwanza.

Ilikuwa ni picha ya watu wawili. Mwanaume na mwanamke. Watu hao wawili walionekana wanatoka kanisani kufunga ndoa. Tayari wameshakuwa wanandoa.

Mwanaume alionekana ni mtu mzima aliyemkadiria kuwa na miaka inayokaribia 60. Alikuwa amevaa suti iliyomkaa vema. Alionekana ama ni mtu tajiri au mwenye madaraka fulani serikalini.

Wa pili ambaye ni bibi harusi, alikuwa ni msichana asiyezidi miaka 25. Alikuwa ni msichana mrembo. Na urembo wake uliongezeka maradufu na vikorombwezo vya mapambo alivyopambwa na wataalam wa kupamba. Picha hiyo kwa hali ya kawaida ilipendeza sana. Ingempendeza yoyote ile ambaye angeiangalia.

Mtu mmoja tu ambaye hakupendezwa na picha hiyo. Ni kadili.

Hakupendezwa kwa sababu moja tu. Bibi harusi aliyeolewa alikuwa anamfahamu. Ni Edina.

"Edina umeolewa?" Ni kama alikuwa anaiuliza picha iliyokuwa kwenye gazeti la Nipashe.

Kuanzia wakati huo, Kadili alionekana kutokuwa kwenye hali nzuri, japo mwenyewe alijitahidi mno kuficha hali hiyo.

"Vipi leo mwanangu, unaumwa?" Mama aliuliza.

"Kwani vipi mama, mbona mzima tu."

"Naona kama hauko vizuri. Nimekuzaa mwenyewe. Nakujua. Kama kuna kitu kinakutatiza mimi najua na hata ukiwa na furaha najua tu, hata kama ukitaka kunificha furaha au huzuni uliyonayo mwanangu."

"Hapana mama uchovu tu."

*****************************

Alipozinduka kwenye usingizi mzito wa mchana, alijizoazoa kivivu na kuokota gazeti lake lililokuwa chini ya kitanda.

Akavaa shati lake na kutoka nje, moja kwa moja hadi kwa rafiki yake Meze.

Baada ya kusalimia, alimkabidhi gazeti, akiwa tayari ameshalikunja sehemu ile ile ya matukio.

Wakati Meze akiangalia picha ile kwa makini kutokana na kutopewa maelezo yoyote ya Kadili ni kwa nini amepewa gazeti la Nipashe ili aangalie sehemu hiyo, mwenyewe alijikuta akijipweteka kwenye kiti kama mtu aliyekosa nguvu.

Meze alilitazama gazeti kwa makini na kugundua nini Kadili alikuwa amekusudia. Macho yalimtoka pima.

"Ameolewa?" Aliuliza. Lakini hakujua nani anamuuliza.

Aliliweka gazeti mezani na kumtazama rafiki yake alivyokaa kwenye kiti kama mtu aliyechoka baada ya kubabashwa mzigo mzito.

"Du pole sana rafiki yangu. Lakini ndiyo yale tuliyokuwa tukizungumza. Ni bora Edina ameolewa ili wewe maisha yako yawe salama. Unajua yule mama sasa atatulia. Hatokufuata tena."

"Ahsante Meze, ila kwa kweli inauma."

"Ndiyo najua, lakini tutafanyaje?"

"Ni kweli, hakuna jinsi. Nakumbuka siku ile kule kwenye jumba lake alivyokuwa anakipiga mkwara, alisema ana watu kibao matajiri, wanasiasa na watu wakubwa wenye hadhi zao wanamiminika kutaka kumuoa binti yake. Kumbe ilikuwa kweli yametimia."

"Haya ni mambo ya mpito tu ndugu yangu Kadili, utapata demu mwenyewe utamsahau Edina, kwanza mtu ambaye hamjawahi hata kuyajenga masuala ya mapenzi, inakuwaje akutie tumbo joto hivi?" Meze aliizidi kumfariji rafiki yake.

**"Naona kama hauko vizuri. Nimekuzaa mwenyewe. Nakujua. Kama kuna kitu kinakutatiza mimi najua na hata ukiwa na furaha najua tu, hata kama ukitaka kunificha furaha au huzuni uliyonayo mwanangu."**

***********************************

Ilimchukua wiki nzima mama Kadili kuelewa somo. Aligundua ndani ya gazeti la Nipashe analopenda kuzurura nalo kijana wake kuna picha ya msichana aliyesababisha kutekwa na kupelekwa asikokujua kwa siku tatu.

Baada ya kijana wake kujisahau na kuacha gazeti, aliitazama picha hiyo ya Edina kuolewa na mwanaume tajiri.

"Haka ndiko kasichana kanakomsababisha kijana wangu matatizo?" Aliangalia kwa makini mwishoni akajisemea. "Mh! Kumbe kazuri. Kana haki. Ila kalitaka kumuua mwanangu, bora kalivyoolewa." Mama Kadili alikuwa akijisemea mwenyewe kimoyomoyo.

Nusu saa baadaye Kadili aliingia na kumkuta mama yake subuleni.

"Shikamoo mama."

"Marahaba Kadili, lakini nina mazungumzo na wewe kidogo."

"Mimi mama."

"Ndiyo wewe sasa nani?"

"Haya." Aliitika na kukaa kwenye kochi."

"Enhee kiko wapi mwanangu." Alianza mama na maneno hayo yalimshtua Kadili.

"Nini kwani mama?"

"Nilikwambia nimekuzaa mwenyewe kwa hiyo ukiwa na furaha hata kama unaificha najua, na hata akiwa na huzuni ukiificha pia najua."

Mpaka wakati huo Kadili hakutaka kuongea lolote, kwani alishajua kuna kitu ambacho mama yake ameshagundua kama kawaida yake.

"Nilikwambia mwanangu, yule msichana ni mtoto wa kitajiri huwezi kumpata, sasa ameolewa na wenye nazo.

Ndiyo maana wiki yote hii hujachangamka. Ameshaolewa, cha kufanya msahau huyo binti, masomo umeshamaliza na sasa umri wa kuoa tayari." Alimeza funda moja la mate akamwangalia kijana wake kwa makini.

"Wiki iliyopita nilikwenda Mtoni Mtongani kwa mjomba wako Polly. Katika maongezi tuliyoongea ni kwamba tumekubaliana wewe umuoe binti yake Eliza."

Habari hiyo mpya ilimshtua Kadili. Anamfahamu Eliza. Ni ndugu yake. Ni mpwa wake. Binti ya mjomba wake aliyezaliwa na mama yake. Ni msichana mrembo na anafaa kuwa mke.

"Mbona Eliza ni mzuri tu, tena huyu ni mtu wetu wa karibu, hatokuumiza kijana wangu."

Kadili hakupinga wala kukubali. Eliza ni msichana mrembo, anayekaribiana na Edina, lakini bado hajamfikia.

Edina alikuwa ni habari nyingine. Kadili hakutegemea kama mama yake anaweza kumwambia jambo kama hilo.

"Sawa mama nimesikia, sijakataa ila ni mapema mno, lakini hilo mlilolimua si baya, ila linahitaji muda."

"Na wiki ijayo atakuja hapa, mwenyewe ameshakubali. Atakuja ili muongee wenyewe, maana sisi tumeshayamaliza."

Kulizuka ukimya wa dakika na ukamalizwa na Kadili mwenyewe.

"Haya." Alijibu.

**Itaendelea Jumamosi**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA / MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA,** NYUMBA INAUZWA SINZA LION KUELEKEA KWA MWAIBULA NYUMA YA DEFRANCE HOTEL, BLOCK E PLOT No. 665, 288 SQM. MAWASILIANO: **0713 525954 / 0787 822000.**

**VIWANJA/NYUMBA.** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Nyumba inauzwa Kaloleni Arusha ina frame za biashara,nyenye SQ 59 mil 800. Nyumba inauzwa Usariver ya bedroom4 mil 70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311



### KUPOTEA KWA CHETI



**IRENE HERIETH F. KIPELEKA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0266/0034** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2015 katika Shule ya Sekondari REGINAMUNDI GIRLS. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **TAN/TAN/RB/9862/2019**

115446402


### KUPOTEA KWA CHETI



**MWATATU CHAVEMBA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S3981.0046** kilichotolewa na MUSTAFA J. SABODO SEKONDARI MWAKA 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MSS/RB/3996/2018.**

115446002


### KUPOTEA KWA CHETI



**IRENE PETER NDEKI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0214/0042** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2011 katika Shule ya Sekondari MSALATO. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **MOR/IFA/RB/336310**

115446302

### PASSPORT IMEPOTEA



**MEJA JUMA KINDIMBO** anatangaza kupotelewa na **PASSPORT No 134737** iliyotolewa 25th Feb 2006 na kuisha 24 Feb 2016. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa polisi: **DOM/RB/781 /2014.**

115446902

### KUPOTEA KWA CHETI



**Esther Donald Victor** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0804-0007** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2012 katika shule ya Sekondari DCT Mvumi. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/CHA/RB/176749/2019**

115446102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;197/2019**

**Ombi la JOSEPH PHILLIP HELLA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu VERONICA ELIA HELLA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 26/09/2019.

215446502

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA KONDOA**

**MAOMBI NA. 27 MWAKA 2019**

**RAMADHANI SALUMU TWAJA...... MUOMBAJI**

**DHIDI YA FATUMA KINJENGELELILE.... MUOMBAJI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA FATUMA KINJENGELELILE**

Fahamu kwa shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 15/10/2019 saa 3 Asubuhi mbele ya Mh. O.MBEGA mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamuriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/Muhuri wa Baraza hii leo 02/10/2019.

115446802

**JAMUHURU YA MUUNGANO TANZANIA MCD/84**

**TANGAZO**

**MAHAKAMA YA MWANZO MAKANG'WA WILAYA YA CHAMWINO –DODOMA**

**MIRATHI NA. 05 YA 2019**

**MUOMBAJI; AMOSI MAKWAWA WA IRINGA MVUMI- DODOMA**

**Kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu CHARLES MAKWAWA aliyekuwa anaishi Iringa Mvumi Dodoma**

Mtu yeyote mwenye pingamizi na mirathi iliyotajwa hapo juu Tanzania Bara na Visiwani. Unatakiwa ulete hilo pingamizi katika Mahakama ya Mwanzo Makang'wa Chamwino Dodoma kabla muombaji msimamizi wa mirathi hajateuliwa ndani ya miezi mitatu.

Tangazo hili limetolewa na Mahakam ya Mwanzo Makang'wa Chamwino Dodoma. Tarehe 03/10/2019

15447002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;199/2019**

**Ombi la HUSNA SELEMANI MUHUNZI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HAMISI SALEHE LIKANDAPAI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 17/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/10/2019.

215447302

### CHAMPION AUCTION MART NOTISI/MNADA

Kwa niaba ya **UNITY 3E SOLUTION (T) LTD MWANZA,** tunatoa **NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14)** kuanzia tarehe ya tangazo hili kwa wadaiwa walio tajwa hapa chini walipe madeni wanayodaiwa kwa muda mrefu.
Endapo watashindwa kulipa kwa muda uliotolewa,dhamana zao zitauzwa kwa mnada wa hadhara kwa ratiba ifuatayo. (1)JINA LA **MDAIWA/MDHAMINI-ISDORY PAUL MJAWA, DHAMANA YAKE- GARI T. 856 BRA (RANGE ROVER TAREHE YA MNADA ITAKUWA- 05/10/2019 SAA 5 ASUBUHI.**
**(2) JINA LA MDAIWA/MDHAMINI- WALTER CHRISTOM MAPUNDA DHAMANA- GARI T 797 DDH (MITSUBISHI) TAREHE YA MNADA-14/10/2019 SAA 5 ASUBUHI.**

**MASHART YA MNADA**
(1) ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili
(2) malipo ni 25% ya bei itakayo fikia kwenye mnada na kiasi kilicho baki kitalipwa ndani ya siku 14
(3) endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa muda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zake na gari /nyumba itauzwa tena.

215446702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;201/2019**

**Ombi la ROSE PASCHAL ROEZEL MAHEDE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu GEORGE ODILLO ROEZER**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 23/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/10/2019.

115447502

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**LOMBURI (TANZANIA LIMITED)** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina **MITSUBISHI CANTER** yenye namba za usajili t158 CGR chassis na **FE517BD433227** Engine na **4D33E451** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/297868/2019**

215447202

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**SALUM SHABANI KAEZE** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T482 DDL.** Aina Yake SUZUKI. Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi, Taarifa ya Polisi: **GAI/B.I/37/VOL.VIII/207**

115447402


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223311**



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# KEANE AZIKATIA TAMAA UNITED, ARSENAL

**LONDON, England**

GWIJI na nahodha wa zamani wa Manchester United, Roy Keane, amesema kwamba hakuna timu yoyote kati ya timu yake ya zamani na Arsenal yenye uwezo wa kuingia ndani ya nne bora msimu huu.

Keane alinukuliwa akisema hayo baada ya kutoridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na klabu hizo zilipokutana katika mchezo wa Ligi Kuu England Jumatatu, ambao zilimaliza kwa sare ya kufungana bao 1-1 katika dimba la Old Trafford.

Ilichukua dakika 28 ndipo shuti la kwanza langoni likapatikana katika mchezo huo, ikiwa ni rekodi ya shuti lililochelewa zaidi msimu huu katika mechi zote za ligi hiyo.

Kiungo Scott McTominay, aliifungia United bao la kuongoza sekunde chache kabla ya mapumziko, lakini Pierre-Emerick Aubameyang alisawazisha kipindi cha pili baada ya VAR kutengua uamuzi ya mwamuzi msaidizi aliyedai mshambuliaji huyo aliotea.

"Tumekuwa tukiangalia mechi za Manchester United na Arsenal na hatuamini jinsi mchezo huu ulivyokuwa mbaya," alisema kiungo huyo wa zamani wa Mashetani Wekundu hao.


"Kulikuwa na upungufu wa ubora, wachezaji walionekana kuwa chini ya kiwango, kadi za njano nyingi, hakukuwa na nidhamu. Lakini upungufu wa ubora unatisha, hakika."

Keane anaamini kuwa timu zote hizo mbili zitafanya kazi ya ziada kuingia ndani kwenye nne bora na kupata nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Alipoulizwa timu ipi itafanikiwa kumpiku mwenzake, Keane alijibu, "Kwa kiwango cha timu hizi, hakuna itakayoingia nne bora.

"United wanatakiwa kuwekeza lakini ukiangalia kiwango chao cha sasa, West Ham na Leicester ndizo zitakazoingia."

# KANE AZUA HOFU SPURS



**LONDON, England**

KLABU ya Tottenham ina hofu kwamba, Harry Kane, anaweza kuomba kuondoka katika kipindi cha majira ya joto mwakani, kwa mujibu wa ESPN FC.

Kane ambaye amelelewa na klabu hiyo tangu utoto wake amefunga mabao 171 katika mechi 262 alizocheza kwenye mashindano yote na kilichopo ni kwamba inadhaniwa anaweza kuchoka kuendelea kuitumikia timu hiyo.

Mkataba wa nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya England utamalizika mwishoni mwa msimu 2023/24, lakini mpango wa mshambuliaji huyo kwa sasa ni kushinda mataji, hivyo huenda akachukua jambo hilo na kutafuta timu itakayompa nafasi hiyo ya kutamba kwenye mataji.

Chanzo kimoja kimeidokeza ESPN FC kwamba, kipigo cha kutoka kwa Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ndicho kinachowatia wasiwasi na kingine ni kutofahamika kwa hatima ya Kocha, Mauricio Pochettino.

Spurs inaamini itavuna zaidi ya pauni milioni 150 kwenye mauzo ya mshambuliaji huyo.

# ALLEGRI KUMRITHI SOLSKJER UNITED

**TURIN, Italia**

KOCHA wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri ameripotiwa kwamba yupo kwenye rada za Manchester United kwa ajili ya kwenda kuchukua mikoba ya kuinoa timu hiyo, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.


Daily Mail limeandika kwamba, Allegri ameanza kujifunza lugha ya kingereza ikielezwa ni mwanzo wa maandalizi yake ya kwenda kutua pale kwenye dimba la Old Trafford.

Kocha wa sasa wa United, Ole Gunnar Solskjaer amekuwa kwenye presha kubwa baada ya kikosi chake kuanza msimu kwa mwendo wa kusuasua, ambapo kwa sasa timu inashika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England baada ya kukusanya pointi tisa katika mechi saba.

Kumekuwa na taarifa kwamba Allegri anaweza kuibukia huko Old Trafford kwenda kuchukua mikoba ya Solskjaer endapo kama mabosi wake watashindwa kumvumilia kutokana na timu hiyo kufanya ovyo.

Mtaliano huo aliacha kazi Juventus baada ya kushindwa kuwapa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini sasa jina lake linatajwa huko Old Trafford na kuaminika kwamba mabosi hao wa United wanaweza kugeukia huduma yake kutokana na uzoefu aliokuwa nao.

Kumekuwa na orodha ya makocha kadhaa wanaohusishwa na kibarua cha United, ambapo ukimweka kando Allegri, wengine ni Mauricio Pochettino na Brendan Rodgers.



HABARI MICHEZO



# NYOTA
## WA NIGERIA AFARIKI MAREKANI

**NEW YORK, Marekani**

MSHAMBULIAJI wa Nigeria, Isaac Promise, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 31.

Taarifa iliyothibitishwa na klabu yake ya Austin Bold ya Marekani, imeeleza kuwa, Promise alifikwa na umauti usiku wa Jumatano, lakini hadi sasa chanzo cha kifo chake hakijaelezwa.

Promise alikiongoza kikosi cha Nigeria kama nahodha, wakati wa michuano ya Olimpiki mwaka 2008 iliyofanyika jijini Beijing nchini China na kufanikiwa kuwa sehemu ya wachezaji waliovishwa medali ya fedha, baada ya timu hiyo kumaliza kwenye nafasi ya tatu.

Muda mwingi wa maisha yake ya kucheza soka aliutumia akiwa nchini Uturuki na klabu za Trabzonspor na Antalyaspor, na baadaye alijiunga na Al-Ahli ya Saudi Arabia kabla ya kwenda Marekani.

Aliyekua beki wa West Ham United, Anton Ferdinand, amekua mmoja wa wanasoka waliotuma salamu za rambirambi baada ya kifo cha Promise.

"Nimeshtushwa," aliandika mkongwe huyo kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram.

"Ulikuwa mwenzangu na tumeishi chumba kimoja tukiwa Antalyaspor. Pumzika kwa amani Isaac Promise. Pumzika kaka."

## Southgate awatema Dele, Lingard England

**LONDON, England**

NYOTA Dele Alli wa Tottenham Hotspurs na Jesse Lingard wa Manchester United, wameachwa kwenye Timu ya Taifa ya England, ambayo itacheza michezo miwili ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Ulaya, Euro 2020, dhidi ya Jamuhuri ya Czech na Bulgaria wiki ijayo.

Kikosi cha England kitaanza kupambana dhidi ya Jamuhuri Ya Czech Oktoba 11 na siku tatu baadaye kitacheza dhidi ya Bulgaria.

Kocha Mkuu wa England, Gareth Southgate, ametangaza kikosi chake na kufanya maamuzi ya kuwaita kwa mara ya kwanza wachezaji wa Chelsea, Fikayo Tomori (beki) na Tammy Abraham (mshambuliaji) huku kiungo wa Everton Fabian Delph akirejeshwa.

Kiungo wa Mabingwa wa Ulaya, Liverpool, Alex Oxlade-Chamberlain ameachwa pamoja na mkali wa Manchester United. Aaron Wan-Bissaka ambaye ni majeruhi.

"Nimefanya mabadiliko kwa kuwaita wachezaji wengine, kutokana na sababu mbalimbali, lakini wengi wao ambao sikuwaita wanakabiliwa na majeraha ama viwango vyao kuwa katika hali ya kawaida," alisema Southgate.



"Ninahitaji kuwa na wachezaji wenye dhima na uwezo wa kupambana, huku wengine tukiwapa wasaa wa kurekebisha kasoro walizonazo, ili tuwaite tena siku zijazo."

Kifuatacho ni kikosi cha England kilichotajwa kwa ajili ya michezo ya kuwania kufuzu fainali za mataifa ya Ulaya dhidi ya Jamuhuri ya Czech na Bulgaria.

**KIKOSI KAMILI**

Makipa: Tom Heaton (Aston Villa), Jordan Pickford (Everton) na Nick Pope (Burnley).

**KIKOSI KAMILI**

Makipa: Tom Heaton (Aston Villa), Jordan Pickford (Everton) na Nick Pope (Burnley).

Mabeki: Trent Alexander-Arnold (Liverpool), Ben Chilwell (Leicester), Joe Gomez (Liverpool), Michael Keane (Everton), Harry Maguire (Manchester United), Tyrone Mings (Aston Villa), Danny Rose (Tottenham), Fikayo Tomori (Chelsea) na Kieran Trippier (Atletico Madrid).

Viungo: Ross Barkley (Chelsea), Fabian Delph (Everton), Jordan Henderson (Liverpool), James Maddison (Leicester), Mason Mount (Chelsea), Declan Rice (West Ham) na Harry Winks (Tottenham).

Washambuliaji: Tammy Abraham (Chelsea), Harry Kane (Tottenham), Marcus Rashford (Manchester United), Jadon Sancho (Borussia Dortmund), Raheem Sterling (Manchester City) na Callum Wilson (Bournemouth).

## Unai ampa mtihani Pepe

**LONDON, England**

NICOLAS Pepe ametakiwa kujifunza kukabiliana na changamoto za Ligi Kuu England, ambayo ameanza kuichezea msimu huu, baada ya kusajiliwa na washika bunduki wa hapa jijini London.

Kauli hiyo imetolewa na kocha wake wa klabu ya Arsenal, Unai Emery, baada ya kutofurahishwa na kiwango alichokionyesha wakati wa mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Manchester United uliomalizika kwa sare ya kufungana bao 1-1, Jumatatu wiki hii.

Pepe mchezaji wa kimataifa wa Ivory Coast aliyesajiliwa kwa dau la pauni milioni 72, amekiri kwamba amekuwa hajiamini kabisa kwa kipindi cha hivi karibuni na hivyo kumfanya acheze kwa kiwango duni hususani katika mchezo huo, ambapo alipoteza mipira mara 17.

Emery amesema mshambuliaji huyo hana budi ajifunze kukabiliana na presha ya ligi hiyo, ili kufanikisha makali yake kama alivyokua Ufaransa na klabu ya Lille.

Kule Lille Pepe alifunga mabao 23 msimu uliopita na hivyo kuwashawishi Arsenal kwenda kunasa huduma yake tena wakilipa mkwanja mrefu uliioweka rekodi huko Emirates.

"Wachezaji nao ni wanadamu, tunacheza michezo kila siku, kama kocha au mchezaji ni lazima kuwa kwenye presha," alisema Unai akinukuliwa BT Sports.

Akaongeza: "Lakini anapaswa kuichukulia presha kwa mtazamo chanya. Kuwa kwenye presha ni kawaida kwa sasa, sisi ni klabu kubwa na tumekuwa na mahitaji makubwa. Hilo ndilo la msingi na si kuzungumzia pesa."

Pepe ameshafunga bao moja katika michezo saba aliyocheza, tangu kuanza kwa msimu huu.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ODEGAARD AZIDI KUGOMBEWA EPL

Guardiola amtaka akabebe mikoba ya Silva, United, Arsenal pia...

**MANCHESTER, England**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu England, Manchester City imeripotiwa kuanza mchakato wa kumwania kiungo, Martin Odegaard ili kuziba nafasi itakayoachwa na mkongwe, David Silva.

Imeelezwa kuwa City ilianza kumfuatilia nyota huyo ambaye ameonyesha kiwango kizuri akiwa na Real Sociedad kwa muda mrefu.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 20 anatajwa kuzifutia klabu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu England baada ya kuisadia Real Sociedad katika mechi mbalimbali, anaitumikia klabu hiyo kwa mkopo akitokea Real Madrid.

Mbali na City, mahasimu wao wa jiji moja, Manchester United pamoja na Arsenal pia wanatajwa kuwania saini ya mshambuliaji huyo raia wa Norway.

City iko katika wakati mgumu kuhakikisha inatafuta mrithi wa mkongwe wake, David Silva, ambaye anatarajiwa kuondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu na tayari Guardiola ameanza kutafuta mchezaji atakayeziba pengo hilo.

Kwa mujibu wa gazeti la El Desmarque, kocha wake anaamini kuwa Odegaard amekuwa mchezaji halisi anayemfahamu baada ya kurejea katika kiwango chake kutokana na kufunga mabao wakati timu yake ikicheza dhidi ya Mallorca na Atletico Madrid.

Kiungo huyo chipukizi kutoka Norway ameichezea mechi mbili tu Real Madrid katika kipindi cha miaka minne na nusu akiwa klabuni hapo, lakini imeelezwa kwamba vigogo hao wa Hispania wanataka kulipwa ada ya pauni milioni 71 ili kumuuza.

Kwa mara ya kwanza alitolewa kwa mkopo msimu wa mwaka 2017/18 kwenda Heerenveen, halafu msimu uliopita aliitumikia Vitesse, lakini sasa amerudishwa Ulaya na kushiriki katika moja ya ligi kubwa duniani.

Hadi sasa msimu huu, Odegaard ameshacheza mechi saba za La Liga, akifunga mabao mawili na amekuwa kwenye kiwango bora kinachovutia kwa muda wote.

Hata hivyo mtandao wa Goal umeandika kuwa Odegaard anataka kuona anarejea Bernabeu baada ya kuwapo na tetesi za kutakiwa klabu mbalimbali za England ikiwamo Liverpool.(Goal)

## KWA UFUPI

**MADRID ILIMTAKA CONTE**

REAL Madrid ilitaka kumwajiri Antonio Conte kuwa kocha wake mkuu hapo mwaka jana, kabla mwalimu huyo wa zamani wa Chelsea hajarejea katika klabu yake ya Inter Milan. ***(Fichajes.net, via Calciomercato)***

**WILSON, MANDZUKIC SOKONI**

STRAIKA wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya England, Callum Wilson (27) na nyota wa Juventus Mcroatia, Mario Mandzukic (33), ni kati ya wachezaji wanaotakiwa na Manchester United katika kipindi cha usajili cha dirisha dogo la Januari. ***(Sky Sports)***

**ERIKSEN KITAELEWEKA**

KIUNGO wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen (27), anaamini kuwa mchakato wake wa kujiunga na Real Madrid utakamilika, huku wakala wa mchezaji huyo anajiandaa kuelekea Hispania wikendi hii ili kufanya mazungumzo na mabosi wa klabu hiyo inayoshiriki La Liga. ***(Star)***

**SARRI AMTAKA WILLIAN**

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Maurizio Sarri, amesema kuwa anaamini ataungana na mshambuliaji wake, Willian katika kikosi cha Juventus, lakini Kocha wa Blues, Frank Lampard, ameweka wazi kuwa klabu hiyo ya Stamford Bridge imeanza mazungumzo ya kumpa mkataba mpya Mbrazili huyo. ***(Calciomercato)***

**MARTINELLI AKWAMA**

MANCHESTER United imesitisha mchakato wa kumsajili straika wa Arsenal, Gabriel Martinelli, ambaye ana umri wa miaka 18 katika kipindi cha majira ya joto, Mbrazili huyo tayari ameshafunga mabao manne katika michezo mitatu aliyoichezea klabu yake. ***(Mirror)***

**CAPELLO: NILIMTAKA MESSI**

KOCHA wa zamani wa Timu ya Taifa ya England, Fabio Capello, ameweka wazi kuwa alijaribu kufanya mchakato wa kumsajili wa mkopo mchezaji nyota wa Barcelona na Argentina, Lionel Messi (32), alipokuwa akiifundisha Juventus. ***(Sky Sports Italia, via Mail)***

**HUGHTON AIKATAA STOKE CITY**

KOCHA wa zamani wa Brighton, Chris Hughton, amekataa ofa ya kwenda kuifundisha Stoke City ambayo inapambana kuhakikisha haishuki daraja katika Ligi ya Championship. ***(Mirror)***

**SANCHEZ KUJADILIWA**

INTER Milan imeweka wazi kuwa haitahusisha majadiliano kuhusu ada ya uhamisho ya Alexis Sanchez itakapozungumza na Manchester United kwa sababu inahofia kumpoteza nyota huyo wa Chile moja kwa moja. ***(Calciomercato)***

**GALAXY YAMTAKA MORELOS**

KLABU ya Los Angeles Galaxy inayoshiriki Ligi Kuu Marekani imeweka wazi nia yake ya kumsajili straika wa Rangers na Timu ya Taifa ya Colombia, Alfredo Morelos, ambaye ana umri wa miaka 23. ***(Star)***

**INCE AGOMBEWA ULAYA**

MABOSI wa Leicester City, wanatarajia kufanya mchakato wa kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Uturuki, Burak Ince (15), ambaye pia anatajwa anawindwa na Manchester City, Lille na Freiburg.***(Fotospor - in Turkish)***

**PODOLSKI AMPIGIA DEBE GNABRY**

MCHEZAJI wa zamani wa Arsenal, Lukas Podolski, amemtania mshambuliaji wa Bayern Munich, Serge Gnabry, anastahili kuwa Mchezaji Bora wa mwezi wa Ligi Kuu England, baada ya Mjerumani huyo mwenye umri wa miaka 24 kufunga mabao manne dhidi ya mahasimu wao wa London Kaskazini, Tottenham Hotspur katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumanne iliyopita. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

# KARUME BOYS KUREJEA KESHO

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya vijana wa umri chini ya miaka 20 cha Zanzibar (Karume Boys), kinatarajia kurejea visiwani hapa kesho kikitokea kwenye mashindano ya Afrika Mashariki na Kati ambayo yalitarajiwa kumalizika jana nchini Uganda, imeelezwa.

Karume Boys ilitolewa katika hatua ya robo fainali baada ya kufungwa mabao 5-0 na Eritrea, lakini ilikwama kutokana na changamoto ya usafiri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Mohammed Ali Hilali, alisema kuwa timu hiyo itawasili majira ya jioni na inaamini kwamba mashindano hayo yamewasaidia kuwapa uzoefu yosso wao.

Hilali alisema kuwa Karume Boys ilikwenda katika mashindano hayo kwa ajili ya kutekeleza programu ya maendeleo ya soka la vijana na si kushindana.

Fainali za mashindano hayo ya U-20, zinatarajiwa kuchezwa leo kati ya yosso wa Tanzania Bara dhidi ya Kenya.

# "MUUAJI" YANGA AITWA KUONGEZA NGUVU STARS

**Na Mwandishi Wetu**

KAIMU Kocha Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije, amemwongeza katika kikosi chake mshambuliaji wa Polisi Tanzania, Ditram Nchimbi, ili kujiandaa na mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Rwanda (Amavubi) utakaochezwa Oktoba 14 mwaka huu jijini Kigali nchini humo.

Nchimbi alifunga "hat-trick" ya kwanza msimu huu wakati timu yake ikitoka sare ya mabao 3-3 dhidi ya Yanga katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Uhuru.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema kuwa kikosi hicho cha Taifa Stars kitakuwa na jumla ya wachezaji 29 na kinatarajia kuingia kambini kesho.

Ndimbo alisema kuwa wachezaji wa Stars wanaocheza nje ya Tanzania wataanza kuwasili nchini zikiwa zimebaki siku chache kama kanuni za Fifa zinavyoeleza.

Alisema kuwa maandalizi kuelekea mchezo huo wa kimataifa yamefikiwa pamoja kati ya TFF na Shirikisho la Soka la Rwanda (Ferwafa), na kila upande unaamini mechi hiyo utawasaidia kiufundi kujiimarisha.

Aliwataja wachezaji wengine 28 walioitwa kwa ajili ya mchezo huo unaochezwa kwenye kalenda ya kimataifa ya Fifa ni pamoja na Juma Kaseja, Metacha Mnata, Said Kipao, Salum Kimenya, Shomary Kapombe, Gadiel Michael, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr', Kelvin Yondani, Erasto Nyoni, Bakari Nondo, Himid Mao, Jonas Mkude, Kelvin John na Farid Mussa.

Nyota wengine walioitwa ni pamoja na Adi Yusuph, Iddi Suleiman, Mudathir Yahya, Salum Aboubakar "Sure Boys",Frank Domayo, Mzamiru Yassin, Shaaban Chilunda, Ayoub Lyanga, Abdul- Aziz Makame, Andrew Simchimba, Miraji Athumani, Feisal Salum "Fei Toto, Simon Msuva na nahodha, Mbwana Samatta.

Stars inatarajia kutumia mechi hiyo ya kirafiki kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa marudiano kuwania tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) dhidi ya wenyeji Sudan utakaochezwa Oktoba 18 mwaka huu kwenye Uwanja wa El Merriekh, Omdurman.

Kikosi hicho cha Ndayiragije kitashuka uwanjani kikiwa na kumbukumbu ya kufungwa bao 1-0 katika mechi ya kwanza iliyochezwa Septemba 22 mwaka huu hapa nchini.



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Walemavu wakifanya mazoezi kwenye Viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam ili kujiandaa na Michezo ya Olimpiki inayotarajiwa kufanyika nchini Kenya hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Azam yaikaribisha Namungo Chamazi

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa zamani wa Kombe la Kagame, Azam FC, wanatarajia kuwakaribisha Namungo FC, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Jaffer Iddi, alisema kuwa kikosi chao kimekamilika na hawana mchezaji ambaye ni majeruhi.

Iddi alisema kuwa wanawaheshimu Namungo na watashuka uwanjani wakiwa na lengo moja la kuzibakisha pointi tatu nyumbani.

"Ni mchezo muhimu sasa, unatarajiwa kuwa na ushindani, tumefanya vizuri sana kutokana na uwezo ambao unaonekana kila Namungo inaposhuka uwanjani.

Aliwataka mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kuwashangilia na kuongeza kuwa Ligi Kuu Bara ni ngumu na timu iliyojiandaa vema ndiyo itakayopata matokeo mazuri.

"Tuna changamoto vizuri sana, kwa spidi kubwa, mchezo wa kupendeza, tumeonyesha kiwango kizuri, hivyo tunatakiwa kucheza vizuri zaidi ya mchezo uliopita," alisema Iddi.

Azam FC ina pointi sita na iko katika nafasi ya tisa kwenye msimamo wakati Namungo wenye pointi saba, wako katika nafasi ya sita.

Ligi hiyo ya juu Bara, inatarajia kuendelea tena kesho kwa wawakilishi pekee wa Tanzania waliobaki kwenye mashindano ya

# Mshindi SportPesa afunguka alivyoshinda

**Na Mwandishi Wetu**

MSHINDI wa Jackpot ya SportPesa ya Sh. milioni 260.3, Scholastika Ngwalueson, ambaye ni mkazi wa Mbagala jijini Dar es Salaam ametaja siri ya ushindi wake wa mamilioni hayo aliyoshinda mara baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 13.

Huyo ni mwanamke wa kwanza kushinda jackpot hiyo tangu SportPesa ianze kuchezeshwa mchezo huo wa kubashiri hapa nchini mwaka 2017.

Washindi wa kwanza kushinda jackpot walikuwa ni Kingsley Pascal kutoka Kagera pamoja na Magabe Matiku kutoka Musoma ambao hao walishinda Sh. milioni 825 na kugawana kila mmoja Sh. milioni 412.

Jinsi alivyoshinda

"Nilianza kucheza na SportPesa muda mrefu nikishirikiana na kaka yangu, Edgar Issaya, ambaye alikuwa akisaidia katika kubashiri mechi mbalimbali.

"Nilikuwa namshirikisha kaka yangu katika kunisaidia kutokana na kuzifahamu timu mbalimbali, hivyo kwa kupitia kwake niliamini nitafanikiwa kama hivyo nilivyofanikiwa.

"Hivyo ushindi huu siyo wa bahati kwangu kuupata, kwani mara kadhaa nilikuwa nikicheza na SportPesa lakini bila ya mafanikio ya kushinda kabla, lakini nilijipa matumaini ya kushinda na nikafanikiwa namshukuru Mungu.

"Kikubwa ninawashauri Watanzania wasikate tamaa pale wanapobashiri mechi zao na pale wanaposhindwa basi wanakata tamaa, kikubwa wao waendelee kucheza zaidi kama ilivyokuwa kwangu.


"Kwani kadiri unavyocheza na SportPesa basi ndiyo unajiwekea mazingira mazuri ya ushindi kama mimi leo hii ni milionea.

Neno kwa SportPesa

"Niwahakikishie Watanzania kuwa hii ni kweli kabisa, SportPesa hawapendelei na nimelithibitsha baada ya mimi kushinda kwani nilikuwa nawaona watu mbalimbali wakicheza na kushinda.

"Hivyo, nimepanga kuendelea kucheza zaidi ya SportPesa baada ya ushindi huu nilioupata ambao kwangu utabadili maisha yangu,"alisema Scolastika ambaye ni muuza Mihogo ya kukaanga Chamazi, Mbagala.

Michezo
Jumamosi Oktoba 5, 2019
Nipashe



## Odegaard azidi kugombewa EPL

HABARI UK 30



Mshambuliaji wa Arsenal, Gabriel Martinelli (kulia), akipambana kumtoka beki wa Standard Liege katika mechi ya Kundi F ya Ligi ya Europa iliyochezwa juzi usiku. Arsenal ilishinda mabao 4-0. **PICHA: MTANDAO**

# SABABU SARE YANGA YATAJWA

Kocha aahidi kuanza rasmi Ligi Kuu kesho dhidi ya Coastal...

**Na Somoe Ng'itu**

UCHOVU na kucheza kwa kutoelewana ni moja ya sababu zilizoifanya Yanga ipate matokeo ya sare ya mabao 3-3 dhidi ya "Maafande" wa Polisi Tanzania katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, Kocha Msaidizi wa Yanga, Noel Mwandila, aliliambia gazeti hili kuwa matokeo hayo ni historia na sasa wataingia tofauti kuwakabili Coastal Union kutoka Tanga, katika mchezo mwingine wa ligi hiyo utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

Mwandila alisema kuwa pia safu yao ya ulinzi haikuwa imara na hali hiyo ilisababisha kuruhusu mabao matatu, baada ya wao kupata goli ya utangulizi katika mchezo huo uliokuwa wa kiporo.

"Nafiriki safu yetu ya ulinzi haikucheza vizuri, haikuwa na maelewano, hatukucheza kama timu, walionekana wamechoka, ilicheza chini ya kiwango na hii ilifanya iruhusu mabao matatu ya haraka, na kusababisha kufanya mabadiliko katika kipindi cha pili, kwa ujumla timu haikucheza vizuri," alisema Mwandila.

Mzambia huyo aliongeza kuwa kikosi chake kilishindwa kufanya mashambuliaji yenye "faida" katika kipindi cha kwanza, lakini wanashukuru kipindi cha pili walibadilika na hatimaye kufunga mabao yaliyosaidia kuondoka na pointi moja katika mchezo huo.

"Kipindi cha pili tulijaribu kulazimisha na kushambulia kwa utulivu kiasi, ilitusaidia na kupata mabao mawili ya kusawazisha, mechi hii imekwisha, sasa akili yetu inajipanga kwa ajili ya mchezo unaofuata," Mwandila aliongeza.

Naye Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Suleiman Matola, alisema kuwa makosa yaliyofanywa na golikipa wake, Kulwa Manzi, ndiyo yaliwafanya wapoteze ushindi.

"Wana bahati sana, kama sio makosa ya kipa wangu, Yanga walikuwa wameshapotea, lakini tunashukuru hatukupoteza mchezo, tutaendelea kujiimarisha kwa ajili ya mchezo unaofuata," alisema Matola.

Yanga yenye pointi moja baada ya kushuka dimbani mara mbili, itaendelea kumkosa Kocha wake Mkuu, Mwinyi Zahera, ambaye anatumikia adhabu ya kufungiwa mechi tatu baada ya kubainika kufanya makosa katika mchezo wao wa kwanza msimu huu walipocheza dhidi ya Ruvu Shooting.

## Simba yaendelea kutamba Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Patrick Aussems amechaguliwa kuwa Kocha Bora wa ligi hiyo kwa mwezi Septemba huku mshambuliaje wake, Miraji Athumani naye ameshinda tuzo ya Mchezaji Bora, imeelezwa.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema jana kuwa Aussems na Miraji wametwaa tuzo hizo baada ya kuwashinda wapinzani wao walioingia nao hatua ya fainali katika uchambuzi uliofanywa na Kamati ya Tuzo ya VPL inayotolewa na shirikisho hilo.

Ndimbo alisema kuwa kwa mwezi huo uliopita, Simba ilicheza michezo mitatu na kushinda yote, ikiifunga Mtibwa Sugar mabao 2-1, Kagera Sugar mabao 3-0 na Biashara United mabao 2-0, ambapo Miraji alikuwa na kiwango kizuri uwanjani kwa mwezi huo na kuchangia kwa asilimia kubwa mafanikio ya timu yake.

"Mbali na kucheza katika kiwango cha juu, Miraji alifunga mabao mawili katika mechi hizo tatu na vile vile alitoa pasi za mabao mawili," alisema Ndimbo.

Aliongeza kuwa Miraji alimshinda mchezaji mwenzake kutoka Simba, Meddie Kagere, ambaye pia alitoa mchango mkubwa katika mafanikio ya Simba ikiwa ni pamoja na kufunga mabao manne na Ismail Kada wa Tanzania Prisons.

"Kada naye, kufuatia mapendekezo kutoka kwa makocha wanaohudhuria mechi katika viwanja mbalimbali, ambavyo ligi hiyo inachezwa msimu huu, alionyesha kiwango kizuri na kutoa mchango katika michezo ambayo Prisons ilicheza, ikishinda miwili, sare moja, ambapo iliifunga Ruvu Shooting mabao 2-1, Mtibwa Sugar mabao 3-1 na kutoka sare ya magoli 2-2 dhidi ya Lipuli FC.

Kwa kutwaa tuzo hiyo, Miraji atazawadiwa kikombe na zawadi ya Sh. milioni moja kutoka kwa wadhamini wakuu wa ligi hiyo, Vodacom pamoja na kisimbusi kutoka Azam TV.

Kwa upande wa Aussems, yeye aliwashinda Mohammed Rishard wa Tanzania Prisons na Abdallah Baresi wa JKT Tanzania, baada ya Mbelgiji huyo kuwaongoza mabingwa watetezi kuweka pointi tisa kibindoni kutokana na mechi tatu walizocheza mfululizo.

Simba ndio vinara wa ligi hiyo baada ya kuwa na pointi 12, wakiwa wamecheza mechi nne wakati watani zao Yanga walioshuka dimbani mara mbili, wana pointi moja na wako katika nafasi ya 19.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >